

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA NNE

Kikao cha Tisa – Tarehe 10 Septemba, 2021

(Bunge Lilianza Saa Nane Mchana)

D U A

Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tukae.

Waheshimiwa Wabunge, leo ndiyo Kikao chetu cha mwisho cha Mkutano huu wa Nne na kwa kuwa Kikao chetu hakitakuwa kirefu sana ningependa tu kuwaalika Wabunge waliloko Msekwa wajijunge nasi kwenye ukumbi huu mkubwa ili kwa pamoja baadaye kidogo tuweze kusikiliza hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu akiahirisha shughuli za Bunge. Kwa hiyo, Waheshimiwa mlioko Msekwa mje moja kwa moja ukumbi mkubwa ili tuwe pamoja kwa sababu Kikao chetu kwa jioni ya leo hakitakuwa cha muda mrefu sana, basi naomba tuwe pamoja katika ukumbi huu.

Sasa Waheshimiwa Wabunge mkiangalia Kanuni zenu mtaona kwamba kuna Kanuni ambayo inaongelea habari ya orodha ya shughuli. Makatibu tukiwa tayari mtanipa *signal...*

Kuna Kanuni ambayo huwa inaongelea orodha ya shughuli, Katibu ni Kanuni ya ngapi ile? Ya thelathini na ngapi? Nadhani ya 36 ukurasa wa 27.

NDG. NENELWA MWIHAMBI, ndc – KATIBU WA BUNGE:
Mheshimiwa Spika, ni ya 36.

SPIKA: Ya 36(5) eeh?

NDG. NENELWA MWIHAMBI, ndc – KATIBU WA BUNGE:
Ndiyo, ukurasa wa 26.

SPIKA: Sawa. Ukurasa wa 26, maana sisi wote ni wanafunzi wa Kanuni kila wakati kwa hiyo, lazima tukumbushane mara kwa mara. Kanuni ya 36(5) inahusu mpangilio wa Shughuli za Bunge. Katika mpangilio wa shughuli za Bunge huwa zinasema, hapana ni ya 36(4)...

Shughuli za Bunge zitaendeshwa kwa mpangilio ufuatao: Kwanza, kuwaapisha Wabunge wapya kiapo cha uaminifu; Pili, kama kuna taarifa ya Rais, hizo zina-take precedence kabla ya shughuli nyingine yoyote. Halafu kama kuna Taarifa ya Spika; halafu kama kuna kuwasilisha ombi; halafu kama kuna hati za kuwasilisha Bungeni, ndiyo maana huwa tunaanza na kuwasilisha hati hapa; halafu maswali kwa Waziri Mkuu na maswali mengine ambayo taarifa zake zimetolewa kabla na kadhalika; Hoja za Mawaziri na kadhalika. Huo ndiyo huwa mpangilio.

Sasa katika mpangilio huo, mtaona shughuli ya kwanza ya Bunge lolote la siku yoyote ya kwanza huwa ni kuwaapisha Wabunge wapya kiapo cha uaminifu, sawa jamani? Kwa kuwa hiyo ndiyo huwa shughuli za kwanza, basi leo tuanze na shughuli hiyo hiyo. (*Makof*)

NDG. NENELWA MWIHAMBI, ndc – KATIBU WA BUNGE:

KIAPO CHA UAMINIFU

Mhe. Dkt. Stergomena Lawrence Tax

(Hapa Mbunge aliyetajwa hapo juu aliapa Kiaapo cha Uaminifu)

SPIKA: Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge.

Baada ya mapema leo kupokea taarifa ya kwamba Mheshimiwa Stergomena Lawrence Tax, ameteuliwa na Mheshimiwa Rais katika nafasi zake zile kuwa mmoja wa Wabunge wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ndio maana tumeanza na shughuli hiyo.

Nichukue nafasi hii kukukaribisha sana na kukupongeza sana kwa kazi kubwa ambayo umemaliza kuifanya ya kuwa Katibu Mkuu wa *SADC*, umetujengea heshima kubwa na tunafarijika sana na tunasikia fahari kubwa kwamba sasa wewe ni mionganini mwetu. Karibu sana nyumbani.

Katibu.

NDG. NENELWA MWIHAMBI, ndc – KATIBU WA BUNGE:
Taarifa ya Spika.

SPIKA: Katibu.

NDG. NENELWA MWIHAMBI, ndc – KATIBU WA BUNGE:

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Maswali, tunaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga, Mbunge wa Mbanga Vijijiini.

Na. 105

**Huduma ya Upasuaji Katika Vituo vya Afya
Mapera na Muungano**

MHE. BENAYA L. KAPINGA aliuliza:-

Je, ni lini Vituo vya Afya vya Mapera na Muungano vitaanza kutoa huduma ya upasuaji ambao haufanyiki kutokana na kukosekana kwa baadhi ya vifaa ikiwemo *sterilizer*?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri, Mheshimiwa David Silinde, tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga, Mbunge wa Jimbo la Mbanga Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 ilipatia Halmashauri ya Wilaya ya Mbanga shilingi milioni 400 kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa Kituo cha Afya Mapera ambapo ujenzi umekamilika na kituo hicho kimeanza kutoa huduma kuanzia Julai, 2021. Mpaka sasa akinamama wajawazito 11 wamekwishanufalka na huduma ya upasuaji.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya Muungano kilianza kujengwa mwaka 2017 kwa nguvu za wananchi na fedha za mapato ya ndani ya halmashauri. Katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 Serikali ilitoa shilingi milioni 60 ili kuendeleza ujenzi wa kituo hicho. Jengo la wagonjwa wa nje (*OPD*) limekamilika na limeanza kutoa huduma kuanzia Julai, 2021. Ujenzi wa jengo la upasuaji unaendelea na upo kwenye hatua ya ukamilishaji.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kujenga na kukarabati vituo vya afya nchini ikiwemo Vituo vya Afya vya Mapera na Muungano ili kuboresha na kuimarisha upatikanaji wa huduma za afya, dawa na vifaa tiba kote nchini.

SPIKA: Mheshimiwa Kapinga, swali la nyongeza, tafadhali.

MHE. BENAYA L. KAPINGA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza nishukuru kwa majibu yanayoridhisha ya Serikali. Ni kweli kituo hiki cha Mapera kuanzia mwezi Julai kimeanza kutoa huduma. Kituo cha Muungano, wananchi

hawa kituo hiki wamekjenga wenyewe kwa asilimia 100 kwa kusaidiwa na mapato ya ndani kidogo sana, hiyo shilingi milioni 60, lakini sasa wanahangaika kujenga jengo la wazazi. Je, Serikali ina mpango gani kuunga jitihada hizi mkono. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Kata ya Kipololo imejenga Zahanati ya Kipololo, Kata ya Mbuji imejenga Zahanati ya Mnyao, Kata ya Litembo imejenga Zahanati Lituru lakini pia Kata ya Mkako Kiukuru wamejenga zahanati. Zahanati hizi zimekamilika, zingine sasa zina miaka mitatu, miwili mpaka leo hazijaanza kazi. Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka watumishi katika zahanati hizi ili ziweze kuanza kufanya kazi? (*Makof*)

SPIA: Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu maswali madogo mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Benaya Kapinga, Mbunge wa Jimbo la Mbinga Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge ameomba tu Kituo cha Afya Muungano ambacho kimejengwa na wananchi kwa asilimia 100 na sasa hivi kuna jitihada za kujenga jengo la wazazi, anataka *commitment* ya Serikali. Niseme tumelipokea na tutaliweka katika mipango inayofuata ili kuhakikisha tunaingiza katika bajeti zetu hiki Kituo cha Afya cha Muungano ili kiweze kukamilika.

Mheshimiwa Spika, la pili kuhusu kata alizozitaja katika vijiji alivyoviainisha kama Kata ya Kipololo, Mbuji, Litembo na Likako ambazo zimejenga zahanati na mpaka sasa hivi bado hazijafunguliwa. Niseme tunalipokea na naamini watendaji wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI ambao wanasimamia Idara ya Afya wamelisikia hili, hivyo sasa tutajua namna ya kupanga watumishi waliopo na vile vile kama Serikali itaajiri hapo mbele kidogo tutapeleka watumishi ili vituo hivi vianze kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na swali linalofuata, Wizara hiyo hiyo, linatoka Kiteto kule kwa Mheshimiwa Edward Olelekaita Kisau.

Na. 106

Hitaji la Shule za Kidato cha Tano na Sita – Kiteto

MHE. EDWARD O. KISAU aliuliza:-

Je ni lini Serikali itapandisha hadhi Shule za Sekondari za Lesoit, Dosidosi, Ndendo na Dongo kuwa Kidato cha Tano na Sita kutokana na uhitaji mkubwa wa Shule za Kidato cha Tano na Sita Kiteto.

SPIKA: Majibu ya swali hilo, bado tupo kwako Mheshimiwa David Silinde, tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Edward Olelekaita Kisau, Mbunge wa Jimbo la Kiteto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali inatambua uhitaji mkubwa wa shule za kidato cha tano na sita katika Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto. Shule tatu ni za bweni na moja ni ya kutwa ambazo zilianzishwa makusudi kwa ajili ya kuwasaidia ndugu zetu wafugaji wanaohamahama ili wasome bila kukatisha masomo. Shule hizo zinashindwa kupandishwa hadhi kutokana na upungufu wa miundombinu ya mabweni, mabwalo na madarasa ya kutosha kwa ajili ya kidato cha kwanza hadi cha nne na kidato cha tano na sita.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kumwagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Kiteto

akishirikiana na wananchi wajenge mabweni, madarasa na mabwalo kwenye shule hizo ili yatosheleze mahitaji ya wanafunzi wa kidato cha kwanza hadi cha nne na kuongeza mengine ambayo yanaweza kutumika kwa ajili ya kidato cha tano na sita ili tuweze kuzipandisha hadhi shule hizo.

SPIKA: Mheshimiwa Edward Olelekaita Kisau, nakuona umesimama, uliza swali la nyongeza.

MHE. EDWARD O. KISAU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mengine mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza, kwa kuwa sasa halmashauri na wananchi kwa kweli wamewekeza nguvu kuboresha miundombinu ya mabweni, vyoo, madarasa, mabwalo katika shule hizo za Dosidosi, Dongo, Ndido na Lesoit, nini *commitment* ya Serikali sasa kama kuwaongezea nguvu katika jitihada hizo za kuboresha miundombinu?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakuwa tayari kwenda na mimi Kiteto kwa siku ambazo sio nyingi sana tutembelee shule hizo za Dongo, Lesoitd, Ndido, Dosidosi na Sunya ili kuona mazingira yalivyo ili tuweze kushauriana? Ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri, David Silinde, tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu maswali madogo mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Edward Olelekaita Mbunge wa Jimbo la Kiteto kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza anataka tu *commitment* ya Serikali kutokana na jitihada kubwa iliyofanywa na wananchi wake katika Jimbo la Kiteto. Nikiri tu kwamba moja ya mpango wa Serikali katika Mwaka huu wa Fedha ni kuongeza upanuzi wa shule 100. Katika hizo shule 100 lengo letu ni ili ziweze kupokea wanafunzi wa kidato

cha tano na cha sita. Kwa hiyo, niseme tu kwamba, miongoni mwa shule tutakazozingatia ni pamoja na maeneo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameainisha katika ule mpango wetu wa shule 100. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, la pili la kwenda Kiteto, nitakwenda. Nitaongozana na Mheshimiwa Mbunge ili tukajionee hayo maeneo husika. Ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa kuwa huwezi kufika Kiteto bila kupitia Kongwa, basi itabidi humo njiani humo pia uangalie shule zenyehi sifa hizo hizo. (*Kicheko*)

Nilikuona Mheshimiwa Leah Komanya.

MHE. LEAH J. KOMANYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa Shule ya Sekondari Ngh'oboko Halmashauri ilishajenga majengo ya kidato cha tano na sita, madarasa manne yakiwa na ofisi tatu na vyoo 16 vya ndani. Je, Serikali iko tayari kujenga bweni na kukamilisha bwalo ambalo liko usawa wa Hanam likiwa na *store* ili shule hii iwe na kidato cha tano na sita? (*Makofii*)

SPIKA: Haya, Wasukuma nao wanataka kusoma. Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri. (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Leah Komanya, Mbunge wa Meatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri Mheshimiwa Mbunge hili ombi lake ameshaliletwa ofisini kwetu na nimeshalikabidhi kwa wataalam waweweze kuangalia kwamba wanaweza kusaidia nini. Maombi aliyoyaainisha hapo ni bweni na bwalo, kwa hiyo, nilishalikubali tangu jana alipokuwa ameniletea yale maombi. Kwa hiyo, nimwambie tu kwamba aondoe wasiwasi, Serikali chini ya Rais wa Awamu ya Sita, Mheshimiwa

Samia Hassan Suluhu itafanya hii kazi na tutaifungua hiyo shule ili wanafunzi waanze kusoma.

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge wa Kinondoni nimekuona.

MHE. TARIMBA G. ABBAS: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Pale katika Jimbo la Kinondoni tuna shule za sekondari tisa zenye wanafunzi zaidi ya 11,000 na *pass rate* pale pamoja na wale wanaokwenda kidato cha tano na sita ni zaidi ya asilimia 80. Hata hivyo, hawa ni watu wa hali ya chini sana, wanapelekwa shule za mbali. Kwa kuwa hatuna *high school*, naiomba Serikali ikubaliane na mimi kwamba itujengee hata *day school* ya *high school* ambayo itaweza kuwasaidia wananchi wa vipato vyta kawaida kabisa katika jimbo lile badala ya kuwapeleka mbali wanafunzi wetu. Ahsante. (*Makof!*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Abbas Tarimba, Mbunge wa Kinondoni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kwamba moja ya maelekezo moja ya maelekezo aliyotoa Waziri wa Nchi katika Halmashauri za Jiji la Dar es Salaam ikiwemo Kinondoni ambazo zina mapato mengi na haya maelekezo tumewaaagiza Wakurugenzi kuhakikisha wanatenga fedha kupitia fedha zao za ndani kujenga shule za sekondari ikiwemo kumalizia madarasa katika maeneo ambayo hakuna.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hili ambalo wameliomba hapa namwagiza Mkurugenzi wa Kinondoni kuhakikisha hili linatekelezeka nami nitakwenda kufuatilia kuhakikisha hii ahadi ambayo nimeiahidi hapa Bungeni inafanya kazi,

Kinondoni wana huo uwezo wa kutekeleza kwa kutumia mapato yao ya ndani. Ahsante.

SPIKA: Siyo nia ujibu sasa hivi, lakini moja ya *interest* yetu ni kujua kwani ni lazima kila *A' Level* iwe bweni? Hatuwezi kuwa na shule za *day* za *A' Level* katika maeneo yetu? Maana itasaidia kweli kweli kurahisisha hizi *A' Level* kuwa katika maeneo mengi. Siyo swali la kujibu lakini ni *interest* ya kuona kwamba zikipatikana hizi shule za *A' Level* za *day* zitaondoa kwanza matatizo mengi na zitawezesha huu ufinyu wa *A' Level*/kupanuka kwa kiasi kikubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Cecilia Parezzo, swali la mwisho kwenye eneo hilo.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuullza swali dogo la nyongeza. Kuna changamoto kubwa sana katika maeneo ya wafugaji; na kwa sababu wana utamaduni wa kuhama; na changamoto hii iko katika baadhi ya Kata katika Wilaya ya Karatu na Mbulu Vijijini katika eneo linaitwa Yaeda Chini; je, Serikali sasa iko tayari kutazama maeneo haya na kuhakikisha wanajenga mabweni kuanzia Shule za Awali, Msingi na hadi Sekondari ili kuhakikisha kwamba jamii hii ya kifugaji na wenyewe watoto wao wanapata haki ya kupata elimu kama ambavyo walivyo katika maeneo mengine nchini? (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri, Mheshimiwa David Silinde tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Cecilia Parezzo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge anaomba kwamba tuendelee kuyazingatia maeneo ya wafugaji na ameainisha hapa eneo la Yaeda Chini na anataka *commitment* ya Serikali ikiwemo kujenga shule kuanzia awali,

msingi na sekondari ili tuweze kuwasaidia maeneo hayo. Nimhakikishie tu kwamba Serikali ya Awamu ya Sita imekuwa ikizingatia kama ambavyo nimejibu kwenye swalii la msingi, katika eneo ambalo anatokea Mheshimiwa Olelekaita, Mbunge wa Kiteto, kwamba Serikali ilijenga kule shule. Kwa hiyo, hata maeneo yote ya wafugaji tutaendelea kuyazingatia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tutaendelea kuyaweka kwenye mpango kwa kadri fedha inapopatikana na kuhakikisha kwamba tunahudumia wananchi wote ili wapate huduma ya msingi ya elimu ikiwemo hayo maeneo ambayo ameainisha. Ahsante sana.

SPIKA: Ahsante. Tunahamia Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, swalii la Mheshimiwa Mbunge wa Nyamagana, Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula.

Na. 107

Masharti ya Ajira kwa Watumishi

MHE. STANSLAUS S. MABULA aliuiliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutimiza masharti ya ajira kwa watumishi ikiwa ni pamoja na kuwapandisha madaraja na stahiki nyingine?

SPIKA: Majibu ya swalii hilo Naibu Waziri, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora) Mheshimiwa Deogratius Ndejembii, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi Umma na Utawala Bora, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula, Mbunge wa Nyamagana, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutimiza masharti ya ajira kwa watumishi wake ikiwemo kupandisha vyeo Watumishi, ambapo Serikali ilitoa barua Kumb. Na. BC.46/97/03D/59 ya tarehe 28 Aprili, 2021 iliyoruhusu upandishwaji vyeo kwa Watumishi wa Umma kuanzia tarehe 1 Juni, 2021. Hadi kufikia tarehe 1 Septemba, 2021, jumla ya Watumishi wa Umma 174,222 wamepandishwa vyeo na kubadilishiwa mishahara yao.

Aidha, Serikali itaendelea kuboresha maslahi kwa watumishi wa umma kadri bajeti itakavyoruhusu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

SPIKA: Mheshimiwa Mabula nimekuona, swali la nyongeza.

MHE. STANSLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru na nitumie nafasi hii kuipongeza sana Serikali ya Awamu ya Sita kwa kuliangalia suala hili kwa kipekee na kulipa uzito na kuwapa matumaini wafanyakazi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nafahamu ya kwamba taasisi nyingi za Serikali zimekuwa na utaratibu wa kuchukua wafanyakazi kwa muda, kwa maana ya vibarua na wengine wanakuwepo kwa mikataba ya muda mfupi. Inapotokea suala la ajira, mara nyingi sana watu hawa wamekuwa wanasahaaulika na kuchukuliwa watu kutoka nje. Kwa mtindo ule ule wa Serikali kuamua kuboresha maslahi ya wafanyakazi, ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha vibarua na wale ambao wana ajira za muda, zinapopatikana fursa wanaajiriwa kwanza wao kama kipaumbele na wengine ndio wanafuata?

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

SPIKA: Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhalii.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula, Mbunge wa Nyamagana, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sera ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma ambayo ilipitishwa mwaka 2008 inaeleza wazi namna ya kupata Watumishi wa Umma kwa njia ya ushindani. Sasa nafahamu kuna maeneo mengi hata majimboni kwa Wabunge wengi kuna watu wengi wanajitolea katika taasisi za Umma.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI Mheshimiwa Ummy Mwalimu alieleza mbele ya Bunge lako hili kwamba kuna *database* ambayo inaanizishwa kukusanya majina ya wale wote amba wanajitolea maeneo mbalimbali nchini ambapo watapewa kipaumbele pale ambapo ajira zitajitokeza. Sasa nitumie nafasi hii kutoa wito kwa wote wale amba wanajitolea kuwasilisha majina yao Ofisi ya Rais, TAMISEMI kama ambavyo alikuwa ametoa maelekezo Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, kwa wale amba hawapo katika ajira za Serikali za Mitaa, wao pia waorodheshe majina yao na kuyafikisha Ofisi ya Rais, Utumishi ili tuweze kuwa na *database* ya pamoja na pale ajira zinapotoka, basi tutaangalia. Kwa sababu kumekuwa kuna *scenario* ambazo watu wanajitolea pale tu wanaposikia ajira zinatoka ili waweze kupata *favour* ya kuweza kuingia kazini. Ili kudhibiti hilo na kuhakikisha ushindani upo katika kuajiri watu katika Utumishi wa Umma, ndiyo maana ajira zile zinatangazwa.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo hao wanaojitolea, naamini watakuwa na *added advantage* kwa sababu wameshaifanya ile kazi kwa vitendo na hivyo wanapoenda kwenye usaili watakuwa wako vizuri zaidi katika kuweza kupata ajira hiyo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante. Tuhamie Maliasili na Utalii, swali la Mheshimiwa Jesca Jonathan Msambatavangu, Mbunge wa Iringa Mjini.

Na. 108

Kujenga Kituo cha Utalii Kihesa – Kilolo

MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Kituo cha Utalii Nyanda za Juu Kusini katika eneo la Kihesa – Kilolo?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Naibu Waziri wa Maliasili, Mheshimiwa Mary Masanja tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jesca Jonathan Msambatavangu, Mbunge wa Iringa Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali iko kwenye hatua za awali za ujenzi wa jengo la kituo cha utalii katika eneo la Kihesa - Kilolo Mkoani Iringa, kupitia mradi wa Kuboresha Usimamizi wa Maliasili na Kukuza Utalii Kusini mwa Tanzania - *REGROW*. Hadi kufikia mwezi Julai, 2021, Wizara imeajiri Mshauri Mwelekezi ambaye anaendelea na kazi ya kutengeneza Mpango wa Biashara na upembuzi yakinifu pamoja na usanifu wa awali wa kituo hicho. Aidha, Mshauri Mwelekezi ameshawasilisha taarifa ya awali.

Mheshimiwa Spika, lengo la kituo hicho ni kutoa huduma za utalii ikiwa ni pamoja na vibali vya kuendesha utalii, kutoa taarifa zinazohusiana na maeneo ya uwekezaji wa utalii na pia kuweka jukwaa kwa sekta binafsi kukaa pamoja na kujadiliana fursa na changamoto mbalimbali katika Sekta ya Utalii ikiwa ni pamoja na kupeana usoefu kwenye kutoa huduma kwa watalii katika sekta hiyo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Jesca nimekuona.

MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nilikuwa nina maswali mawili ya nyongeza. Swali langu la kwanza, Serikali ina mpango gani pia kuendelea kutoa vibali kwa ajili ya wale wawindaji waliokuwa wakifanya uwindaji katika mbuga zetu za nyanda za juu kusini?

Mheshimiwa Spika, pia Serikali ina mkakati gani wa kushirikiana na Wizara ya Fedha ili kuboresha huduma za upatikanaji wa fedha za kigeni ili kuwarahisishia watalii nchini hasa kwa kuruhusu maduka ya kubadilisha fedha za kigeni?

SPIKA: Majibu ya maswali hayo mawili, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Jesca Jonathan Msambatavangu, Mbunge wa Iringa Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge ameulizia kuhusu vibali vya uwindaji. Vibali vya uwindaji vimeendelea kutolewa na Wizara kama kawaida na wafanyabiashara kwa maana ya wawekezaji wote ambao wanatamani kuja kuwekeza kwenye eneo hili la uwindaji, tumekuwa tukitoa vibali kuititia mbinu mbalimbali ikiwemo ya kuititia manunuzi ambayo tunatangaza kwa njia ya kieletroniki. Kwa hiyo, ninawaalika tu wawekezaji ambao wanataka kuwekeza katika sekta hii ya uwindaji waje na kila baada ya muda tunapokuwa tumefanya matangazo haya kuna ambao wanapata lakini wanaochelewa, tunaendelea kutangaza kila baada ya muda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwenye upande wa kubadilisha fedha kwenye maduka haya ya fedha za kigeni, mpaka sasa Serikali imeendelea kushirikiana na hao wafanyabiashara

ikiwemo kuandaa mazingira mazuri kwa ajili ya kuendelea na biashara hii ya kubadilisha fedha. Tunawaomba tu wale wafanyabiashara wote ambao wanafanya biashara hizi waendelee kufuata taratibu wa Serikali kama ambavyo imeendelea kuelekezwa na Wizara ya Fedha. Nasi Sekta ya Maliasili na Utalii tutaendelea kuungana nao pamoja ili kuhakikisha kwamba biashara hii inaendelea kufanyika ili tuweze kukuza utalii katika nchi yetu. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Tuendelee na swali linalofuata la Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto la Mheshimiwa Dkt. Alice Karungi Kaijage. Mheshimiwa Dkt. Alice uliza swali lako.

Na. 109

Mpango wa Kukarabati Hospitali ya Mirembe

MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati Hospitali ya Wagonjwa wa Afya ya Akili ya Mirembe ambayo Miundombinu yake imeharibika?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Dkt. Mollel tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA WAZEE NA WATOTO alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Alice Karungi Kaijage, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kumtumia Wakala wa Majengo (*TBA*) imeanza upembuzi yakinifu wa majengo yatakayofanyiwa ukarabati pamoja na yale yatakayobomolewa na kujengwa upya. Aidha, kuititia upembuzi huo Serikali itabaini gharama halisi za ujenzi na

ukarabati wa Hospitali hiyo. Kazi hii inatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Oktoba, 2021.

SPIKA: Ahsante kwa jibu fupi. Mheshimiwa Dkt. Alice.

MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza; nafahamu kwamba utaratibu wa kuomba fedha kwa awamu ya kwanza ya ukarabati umeshakamilika. Swali langu langu kwa Serikali: Je, ni lini fedha hizo zitatolewa ili ukarabati uanze?

Swali la pili: Je, Serikali ina mpango gani wa ziada kuhakikisha kwamba ukarabati wa majengo haya chakavu ya Milembe unakamilika katika awamu hii na awamu ijayo ya mwaka wa fedha?

SPIKA: Majibu ya maswali hayo muhimu kabisa mawili ya nyongeza Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA WAZEE NA WATOTO (MHE. DKT. GODWIN O MOLLEL): Mheshimiwa Spika, kama ambavyo amesema Mheshimiwa Mbunge, ni kweli kwamba kuna utaratibu ambao tayari umefanyika, lakini wakati utaratibu huo umefanyika imeonekana kwamba kwa kweli unahitajika ukarabati mkubwa sana na vile vile baadhi ya majengo kubomolewa na kujengwa upya, kwa hiyo, ikahitajika kufanyika tathmini kwa sababu fedha nyingi zitahitajika zaidi.

Mheshimiwa Spika, mara tu baada ya huu upembuzi kufanyika, kwanza kazi ambayo ilikuwa inaendelea itaendelea kufanyika, lakini tunahitaji ifanyike kazi kubwa zaidi kwa maana ya kuingia kwenye bajeti ya mwaka kesho 2022 ili ujenzi mkubwa ufanyike na ukitambua kwamba pale Mirembe inaenda kuwa taasisi kamili, sasa iko kwenye wakati wa kuunda muundo. Maa yake kutakuwa na ongezeko la kibajeti na wataweza sasa kuandika *proposal* zao binafsi ili

kufanya *research* na pengine ile taasisi kuwa kubwa zaidi kuliko ilivyo sasa. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, utafiti unaonyesha wagonjwa wengi sana wanaokuja Milembe wanatokea maeneo ya Tabora, Shinyanga, Geita Mwanza; sasa si lifunguliwe tawi lingine huko! (*Kicheko/Makofi*)

Nimemwona Mheshimiwa Nape anataka aongeze swali la nyongeza. Mnahitaji Kusini pia, swali la nyongeza tafadhali.

MHE. NAPE M. NNAUYE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Sisi Kusini nadhani magonjwa haya kwa sababu ya korosho hayapo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya aliwahi kutembelea kusini. Katika ziara yake, tulimpa maombi ya kusaidiwa kukarabati kituo cha afya kikongwe kuliko vyote katika Jimbo la Mtama ambacho kinahudumia zaidi ya kata sita na ahadi hiyo ilitolewa. Sasa nataka kujua ni lini tutapata fedha ili tusaidie kuboresha huduma katika eneo hili?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA WAZEE NA WATOTO (MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nape, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kweli kama ambavyo amesema tulikwenda na vilevile baada ya hapo aliandika barua kwa Mheshimiwa Waziri wa Afya na Mheshimiwa Waziri wa Afya aliwasiliana na TAMISEMI. Nataka kumhakikishia kwamba kituo hicho kimeingizwa kwenye bajeti na kimetengewa shilingi milioni 500 na baada ya fedha kupatikana kazi itaanza. Nami baada ya kumaliza Bunge, twende pamoja ili tusisitize na mambo mengine ambayo tuliyapanga wakati ule kuyafanya. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Bado tuko Afya, swali la Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke.

Na. 110

Kuwezesha Maafisa Maendeleo ya Jamii

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE aliuliza: -

Je, ni kwa kiasi gani Serikali imewezesha Maafisa Maendeleo ya Jamii ambao wamepewa jukumu kubwa la kuanzisha na kusimamia shughuli za vikundi nya Maendeleo kwenye Halmashauri ili waweze kutimiza majukumu yao ipasavyo?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, bado tuko Afya. Ndiyo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya upande wa Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Mwanaidi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,
WAZEE NA WATOTO (MHE. MWANAIDI ALI KHAMISI)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inawezesha Maafisa Maendeleo ya Jamii kupata vitendeakazi kadri Bajeti inavyoruhusu, ambapo hadi sasa imewapatia pikipiki 29 Maafisa wa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino Mkoani Dodoma na Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika Mkoani Katavi.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI imetoa kanuni za utoaji na usimamizi wa mikopo kwa vikundi nya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, marekebisho haya ya mwaka 2021. Kupitia kanuni hii, Maafisa hawa hutengewa fedha kutoka kwenye marejesho kwa ajili ya ufuatiliaji wa mikopo hiyo.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Josephine swalii la nyongeza.

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swalii moja la nyongeza. Kutokana na majibu yaliyotolewa na Serikali, inaonyesha ni dhahiri ni Halmashauri mbili tu kati ya Halmashauri 184 nchi nzima ambazo zimepatiwa pikipiki. Hali hii inaonyesha jinsi ambavyo upo uhitaji mkubwa katika Halmashauri nyingine. Je, Serikali ina mkakati gani wa makusudi kuhakikisha kitengo hicho kinawezeshwa kibajeti katika Halmashauri zote? (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya swalii hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya na Maendeleo ya Jamii.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,
WAZEE NA WATOTO (MHE. MWANAIIDI ALI KHAMISI):**
Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Josephine kwa kufuatilia Maafisa hawa na kuona umuhimu wa kazi zao wanazozifanya.

Mheshimiwa Spika, ni kweli Maafisa hawa wana changamoto kubwa ya vitendea kazi. Mimi mwenyewe binafsi baada ya kumalizika Bunge la Bajeti niliweza kutembelea mikoa mitatu pamoja na Wilaya zake, yaani Mkoa wa Tabora, Iringa na Ruvuma na nimekutana na Maafisa hawa wa Ustawi wa Jamii wakanielezea changamoto zao.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Wizara inaendelea na mikakati ya kuwasiliana na wadau wa Maendeleo ya Jamii ili pamoja na miradi ambayo wanaitekeleza na wadau hao, kuwawezesha Maafisa hawa wa Jamii kuendelea kupata vifaa vyia kufanyia kazi kulingana na mazingira yao waliiyokuwa nayo.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inawajali sana wafanyakazi pamoja na wananchi wake. Kwa hili tumelipokea na tutaendelea kulifanyia kazi suala hili la upatikanaji wa vitendea kazi kwa mikoa yote nchini Tanzania. Ahsante, napenda kuwasilisha.

SPIKA: Mheshimiwa Condester nimekuona.

MHE. CONDESTER M. SICHALWE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa fursa hii.

Mheshimiwa Spika, kutohana na uhalisia kwamba halmashauri zetu nyingi nchini zina changamoto sana ya miundombinu. Serikali haioni kuna haja ya kubadilisha usafiri kutoka kwenye pikipiki na kuwapatia magari maafisa maendeleo ya jamii hawa ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa urahisi na kwa uwanda mkubwa? Kwa mfano, kipindi cha mvua mtu huyo atatumiae pikipiki maana yake atakuwa analowa, hawezi kutekeleza majukumu yake. Serikali haioni umuhimu wa kuwanunulia magari maafisa maendeleo ya jamii ikiwa ni pamoja na Jimbo la Mombasa?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Maendeleo ya jamii

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,
WAZEE NA WATOTO (MHE. MWANAIDI ALI KHAMIS):**
Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali moja la nyogeza la Mheshimiwa Condester kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli, maafisa hawa wanatembea kwa pikipiki kwa ajili ya kufuatilia wafanyakazi hawa au vitendo mbalimbali vinavyotokea katika jamii. Serikali kama nilivyoleza imejipanga kuzungumza na wadau ambao wanaendeleza maendeleo haya ya jamii ili kuhakikisha kwamba maafisa hawa hawatopata tabu katika kazi zao katika mazingira yao ya kazi kwa mujibu wa sheria zilizopo, ahsante nashukuru. (*Makof!*)

SPIKA: Ahsante sana, Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate tafadhali.

Na. 111

Kusambaza Umeme wa REA – Tunduru Kusini

MHE. DAIMU I. MPAKATE aliuliza:-

Je, ni lini Mkandarasi wa umeme wa *REA* ataanza kazi ya kusambaza umeme katika Jimbo la Tunduru Kusini?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Nishati.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI alijibuu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, Mbunge wa Tunduru Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kuitia Wakala wa Nishati Vijiji (REA) imeanza kusambaza umeme nchini kuanzia Mwezi Mei, 2021 ambapo Kampuni ya *M/S Guangdong Jianneng Electric Power Engineering Co. LTD* imepewa kazi hiyo katika Wilaya ya Tunduru ikiwa ni pamoja na Jimbo la Tunduru Kusini.

Mheshimiwa Spika, kazi za mradi zinahusisha ujenzi wa kilomita 639 za njia ya umeme ya msongo wa kilovoti 33, njia za umeme msongo wa kilovoti 0.4 yenye urefu wa kilomita 80, ufungaji wa transforma 80 na uunganishaji wa wateja wa awali wapatao 1,760. Gharama ya mradi ni shilingi bilioni 36.67.

Mheshimiwa Spika, Mkandarasi kwa sasa anakamilisha usanifu wa kina na uletaji wa vifaa vya ujenzi wa miundombinu ya umeme. Mradi unatarajiwaa kukamilika Mwezi Desemba, 2022 na kufikisha huduma ya umeme katika

vijiji vyote 80 vilivyokuwa vimebaki bila umeme katika Wilaya ya Tunduru.

SPIKA: Mheshimiwa Daimu Mpakate nimekuona.

MHE. DAIMU I. MPAKATE: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri wa Nishati na ni kweli mkandarasi yupo site anaendelea na kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa vijiji 11 vya awali vilivyopata umeme awamu ya kwanza, ya pili na ya tatu umeme ule ulipita barabarani bila kupita mitaa yote katika vijiji hivyo kama ville ilivyo Azimio, Chiwana, Mbesa pale Tuwemacho na Ligoma. Ni lini sasa Serikali itaona haja ya kupeleka kuanza mradi wa ujazilizi katika vijiji hivyo ili vitongoji vyote vilivyopo kwenye vijiji hivyo vipate umeme.

SPIKA: Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri Byabato tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza ya Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, Mbunge wa Tunduru Kusini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba *plan* na maelekezo ya Serikali ni kuhakikisha kwamba vijiji vyote 12,268 vinapata umeme iflikapo Desemba mwakani na hilo sisi kwa kutekeleza maelekezo ya Serikali tunaiahidi umma kwamba tutakamilisha maelekezo hayo kwa kadiri ilivyoelekezwa na ilivyoazimiwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo la vitongoji, upelekaji wa umeme kwenye eneo la vitongoji ni zoezi endelevu ambapo wenzetu wa *TANESCO* wanaendelea kupeleka umeme katika maeneo hayo lakini pia vipo vitongoji vingi ambavyo vitaguswa na Mradi huu wa *REA III round two*. Lakini *specifically* upo mradi wa vitongoji ambaao ni wa *densification* yaani umeme jazilizi ambaao tunatarajia uanze mwenzi wa 10 mwishoni ambaao utahusika pia katika kipeleka

umeme kwenye vitongoji alivyovitaja katika Jimbo la Tunduru Kusini. Nashukuru.

SPIKA: Mheshimiwa Festo Sanga nimekuona

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimiwa Spika, ahsante, changamoto ambayo ipo kwa Mheshimiwa Mpakate kuhusu umeme wa *REA* pia ipo Makete ambapo mkandarasi aliyemaliza kutekeleza mradi wake ye ye anasema amemaliza lakini bado tuna changamoto ya kwamba kuna Vijiji kama Mago, Mbela na Kinyika ambako tuna zaidi ya nyumba 1,000 ambazo wananchi wameshasuka umeme toka 2019 lakini hadi ninavyozungumza muda huu wananchi hao hawajaingiziwa umeme kwa sababu ya kwamba mita na nguzo zimeisha.

Je, ni ipi kauli ya Serikali kwa huyu Mkandarasi wa *REA* ambaye hajakamilisha kazi yake ipasavyo ndani ya Jimbo la Makete na wananchi wangu wanaendelea kuteseka? Ahsante. (*Makof!*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Stephen Byabato tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Festo Sanga, Mbunge wa Makete kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tunapompatia mkandarasi kazi, tunampa wigo wa kufanya kazi ambayo tunaita ni wateja wa awali. Na kwa wakandarasi wa *REA III Round One* wako wakandarasi kama wanen ambao walikuwa hawajakamilisha kazi zao ambao tumewaelekeza ifikapo mwishoni mwa mwezi wa 10 wawe wamekamilisha kazi zote. Hivyo, tunatarajia kuanzia mwezi wa 11 hakutakuwa kuna mkandarasi ambaye alikuwa anafanya kazi tofauti na *REA III Round Two* ambaye atakuwa bado yupo kazini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba baaada ya hapa nitafuatilia

na kujua hivyo vijiji vilivyobaki ni vingapi na avikamilishe kwa sababu kwenye *REA III Round Two* hatutaacha kijiji hata kimoja ambacho hakitapata umeme ifikapo Desemba mwakani. (*Makofi*)

SPIKA: Tuendelee na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, swali la Mheshimiwa Mwantumu Mzamili Zodo, Mheshimiwa Mwantumu tafadhali.

Na. 112

Uboreshaji wa Mazingira ya Uvuvi

MHE. MWANTUM M. ZODO aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha mazingira ya Wavuvi wa ukanda wa Pwani ili kuchochaea uchumi?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Abdallah Ulega tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwantum Mzamili Zodo, Mbunge - Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha mazingira ya wavuvi wa Ukanda wa Pwani, Serikali inafanya yafuatayo:-

(i) Serikali imeweka mazingira rafiki kwa wavuvi kupata mikopo ya masharti nafuu kutoka taasisi mbalimbali za fedha;

(ii) Kupitia ufadhili wa *Shirika la IFAD*, Serikali inaboresha masoko ya mazao ya uvuvi pamoja na kuweka miundombinu wezeshi ya kupunguza upotevu wa mazao ya uvuvi na;

(iii) Kupitia Taasisi ya Utafiti a Uvuvi (*TAF/R*), Serikali inatarajia kuweka vifaa vya kuvutia samaki katika Bahari ya Hindi kwa ajili ya kusaidia wavuvi kupata samaki kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali inaendelea na programu ya kuainisha maeneo yenye uvuvi wenyewe tija kwa kutumia *satellite* ili kuwataarifu wavuvi maeneo ambayo samaki wanapatikana kwa wingi, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Mwantumu uliza swali lako la nyongeza.

MHE. MWANTUMU M. ZODO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali itajenga soko kuu la kuuzia samaki kwa Mkoa wetu wa Tanga na ni lini ujenzi utaanza?

Mheshimiwa Spika, swali namba mbili; ni upi mkakati wa Serikali wa kuhakikisha wavuvi wa maeneo ya pembezoni kwa maeneo ya Moa, Chongoleani, Kipumbwi na Mkoaja kuuza samaki wao kwenye soko la pamoja kukwepa wachuuzi kuwachuza kwa bei ndogo? ahsante.

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mwantumu Zodo, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Tanga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika majibu ya msingi nimeeleza kwamba kwenye bajeti ya mwaka huu na kupitia ufadhili wa Shirika la *IFAD*, upo mpango wa Serikali wa kujenga masoko ya samaki. Na soko hili litajengwa katika Wilaya ya Pangani katika Kijiji cha Kipumbwi litakuwa ni soko zuri kubwa na la Kimataifa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ameuliza je watauzia wapi wavuvi wa Chongeleani, Mkinga, Kipumbwi na kwingineko. Naomba nimhakikishie kwamba soko hili litakapokuwa tayari, wavuvi wa maeneo yote aliyoyataja watafaidika kwa ajili ya kuuza bidhaa zao, ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Felister nilikuona.

MHE. FELISTER D. NJAU: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, wavuvi wengi wadogowadogo katika ukanda wa Pwani Jimbo la Kawe hasa katika Kata za Msasani, Kawe, Mbweni na Kunduchi wanachangamoto kubwa ya mtaji wa kununua vifaa vya kisasa stahiki ambavyo vinaweza kuwasaidia kupata samaki kulingana na taratibu za kisheria. Ni nini mkakati wa Serikali katika kuhakikisha wavuvi hawa wanapata vifaa hivyo? Ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo, bado tupo kwako Mheshimiwa Naibu Waziri Abdallah Ulega tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza kutoka kwa Mheshimiwa Njau kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mtaji kwa wavuvi ni moja ya Sera yetu ya Serikali na Serikali ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan imesisitiza katika kuweka mazingira rafiki ili kusudi wavuvi wetu waweze kupata mikopo.

Mheshimiwa Spika, katika hili, kwa kutumia dirisha liliopo Benki yetu ya Kilimo, iko mikopo kwa ajili ya wavuvi na wadau wanaoshughulika na masuala ya uvuvi.

Mheshimiwa Spika, naomba nimuombe Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wengine wote wanaotoka katika maeneo ya wavuvi kuhakikisha kwamba wavuvi wanakaa katika vikundi. Na sisi tupo tayari kwenda kuwaunganisha na mabenki na hata kuwapa elimu na mpango mkakati wa namna ya kuandika kuweza ku-access fursa ile ya kupata mikopo, ahsante sana.

SPIKA: Bado tupo Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Aida Khenani sasa uliza swali lako tafadhali.

Na. 113

Mkopo kwa Vikundi vya Wavuvi

MHE. AIDA J. KHENANI aliuliza: -

Je, Serikali imesaidia mikopo kwa vikundi vingapi vya wavuvi Wilaya ya Nkasi?

SPIKA: Majibu ya swali hilo bado tupo kwako Mheshimiwa Abdallah Ulega tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, Mbunge wa Nkasi Kaskazini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika llani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020 – 2025 Ibara ya 43(h) inaelekeza Serikali ihamasishe uanzishaji na uimarishaji wa vikundi na Vyama vya Ushirika vya Msingi vya Wavuvi wadogo kwa lengo la kuwapatia mitaji, ujuzi na vifaa pamoja na zana za uvuvi. Katika kutekeleza ahadi hiyo, Serikali imefanya yafuatayo:-

(a) Imeendelea kuhamasisha wavuvi kujiunga kwenye Vyama vya Ushirika vya Wavuvi ambapo kwa mwaka wa fedha 2020/2021 jumla ya wadau 16,733 kutoka halmashauri 21 nchini wamepatiwa mafunzo hayo ikiwemo halmashauri ya Wilaya ya Nkasi ambapo hadi sasa jumla ya Vyama vya Ushirika 146 vya Wavuvi vimeundwa.

(b) Serikali imeendelea kuwezesha wavuvi kuitia Vyama vya Ushirika vya Wavuvi kwa kuvipatia injini za boti, ambapo kwa sasa Serikali ipo kwenye mchakato wa kuvipatia injini za kupachika Vyama vya Ushirika vya Wavuvi

kumi kikiwemo Chama cha Ushirika Kabwe kilichopo Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Aida, nimekuona swalii la nyongeza.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuuliza maswali, naomba niishukuru Serikali kwa kunipatia injini siku ya leo Kata ya Kabwe, ninawashukuru sana. Nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:- (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Naibu Waziri amenukuu llani ya Chama Cha Mapinduzi Ibara ya 43(h), natambua kwamba llani hiyo hajasema tukawatie umasikini Watanzania/wavuvi, imeelekeza mkawapatie mitaji na mikopo. Watu wa Nkasi shida yetu sio llani ila llani isipotekelizwa hapo ndipo maswali yanakuja. Ni lini llani Ibara ya 43 itatekelezwa Wilaya ya Nkasi kwa kuwapatia mikopo wavuvi wa Ziwa Tanganyika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swalii langu la pili; kupitia llani hiyo hiyo, nimesoma mwanzo mpaka mwisho hakuna sehemu llani imesema tukawape umasikini Watanzania. Kwa kuwa baada ya operesheni ya uvuvi haramu, Watanzania hasa wavuvi wa Nkasi wamekuwa maskini. Ningependa kujua, nini mkakati wa Serikali kwa kuwapatia vifaa vya kisasa ili kuwaondoa wavuvi hawa katika umasikini. (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo tafadhali Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Aida Khenani kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, la kwanza; ninapokea shukrani kwa niaba ya Serikali na Wizara yetu ya Mifugo na Uvuuvi

uliyoitoa Mheshimiwa Aida Khenani kwa kuwawezesha wavuvi wa Kikundi cha Ushirika cha Kabwe.

Mheshimiwa Spika, lini tutatoa mitaji? Naomba Mheshimiwa Mbunge yeye na wataalam wetu waliopo kule Halmshauri ya Nkasi kwa pamoja tushirikiane katika kuhakikisha kwamba tunaandaa sasa utaratibu wa vikundi hivi kuweza kupata fomu, kuzijaza, waainishe, wapewe elimu kwa kusudio la kuweza kuwaunganisha na Benki ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Aida Khenani, nipo tayari kabisa kuhakikisha kwamba tunasimamia jambo hili katika kutekeleza llani makini kabisa ya Chama Cha Mapinduzi ili kusudi wananchi hawa waweze kupata mikopo hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili; ni kwa namna gani tutawasaidia mara baada ya kufanya operesheni ambayo yeye Mheshimiwa Mbunge anaitamka kwamba imewatia umasikini. Nataka nikuhakikishie kwamba kwanza operesheni ile ilikuwa ni kwa mujibu wa Sheria ya Uvuvi na matokeo ya operesheni ile wengi wameyavutika kwa sababu tulipata samaki wengi, wakubwa na wazuri.

Mheshimiwa Spika, na sasa namna ya mpango tulionao wa namna ya kuwasaidia, moja ni hili tulilolifanya leo kwa kukukabidhi mashine itakayokwenda kuwasaidia watu wa kule Kabwe. Na ninakupa hamasa wewe na Wabunge wengine wanaotoka katika kanda ya uvuvi watuletee maombi zaidi ili kusudi Serikali tuweze kusaidiana nao. Na dirisha la Benki ya Kilimo liko wazi, sisi tunacho kitengo maalum cha kuweza kusaidiana na wavuvi kuandika programu zile na kwenda kuomba zile pesa ili waweze kununua zana bora na waweze kufika mahala mbali kunapoweza kuwasaidia kupata mavuno toshelevu na biashara nzuri, ahsante sana.

SPIKA: Ahsante sana, ahsante. Tunahamia Kilimo kwa sababu ya muda, Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Hazara Chana tafadhalii.

Na. 114

Kuwaunganisha Wakulima wa Wawekezaji wa Nje na Ndani

MHE. BALOZI DKT. PINDI H. CHANA aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwaunganisha Wakulima wa Mikoa ya Kusini hususan Mkoa wa Njombe na Wawekezaji wa nje na ndani?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Kilimo, Mheshimiwa Mohamed Bashe.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Pindi Hazara Chana Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu mkubwa wa kuwaunganisha wakulima na wawekezaji wa ndani na nje ili kuwa na mfumo endelevu unaowapa fursa ya wote kuwepo na kwa faida ya pande zote mbili. Katika kutekeleza mpango huo, Serikali kupitia Wizara ya Kilimo imekuwa inaratibu makubaliano kati ya wanunuzi/wasindikaji na wakulima kupitia kilimo cha Mkataba kwa ajili ya kurahisisha upatikanaji wa teknolojia, pembejeo pamoja na masoko.

Mheshimiwa Spika, kupitia ushoroba wa maendeleo wa *SAGCOT*, Wizara imehamasisha wawakezaji *Tanzania Agrofood Ltd & Olivado Ltd* katika Mikoa ya Njombe na Iringa ambao wameunganishwa na wakulima wadogo na kuwezesha kuongezeka kwa mauzo wa mazao mbalimbali mfano parachichi. Mauzo yameongezeka kutoka tani 3,696 mwaka 2015 hadi tani 7,190 mwaka 2019.

Aidha, bei parachichi pia imeongezeka kutoka shilingi 1,200,000 kwa tani mwaka 2015 hadi shilingi 1,800,000 kwa

tani mwaka 2020. Uwepo wa kampuni hizo zinazowahakikishia wakulima soko imekuwa ni chachu ya kuongezeka kwa uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, Serikali kuititia *program* ya *Agri-connect* inayotekelizwa kwa uratibu wa Wizara ya Kilimo moja ya nguzo zake ni kuunganisha wakulima na wewekezaji katika mnyororo wa thamani. Programu hiyo katika Mikoa ya Kusini ukiwemo Mkoa wa Njombe ambapo mazao ya kipaumbele ni mazao ya bustani, chai na kahawa. Programu hiyo inalenga kuwaunganisha wakulima na masoko ya ndani na ya nje.

SPIKA: Mheshimiwa Balozi nimekuona.

MHE. BALOZI DKT. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri sana ya Serikali hususan kuhusu zao la parachichi, bado mikoa ya Kusini hususan Njombe, zao la mahindi limeendelea kuwa ni changamoto. Serikali ina mpango gani wa muda mrefu wa kuondokana na hii changamoto ya zao la mahindi? Ikiwa ni bei ya mahindi pamoja na changamoto ya mbolea kwa Mkoa wa Njombe na Mikoa ya Kusini?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Chana, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, moja; Serikali kuititia Wizara ya Kilimo tukishirikiana na wenzetu wa Wizara ya Viwanda na Biashara tumeamua sasa hivi kubadili mfumo wa uuzaaji wa mazao ya kilimo badala ya kusubiri wanunuzi kuja ndani ya mipaka ya Tanzania sasa tunawafuata katika maeneo yao. Serikali sasa hivi imeanza mchakato wa kufungua maghala katika baadhi ya nchi ikiwemo nchi ya *South Sudan*, tunafungua ghala letu la kwanza kwa ajili ya kuuza mazao, ghala hilo litatumika vilevile na *private sector* pale ambapo *private sector* wanataka kuuza. Vilevile tunafungua ghala la

kuuza mazao ya chakula katika Jiji la Nairobi kwa ajili ya kuuza *processed products* kwa maana ya unga wa mahindi, mchele na mafuta ya kula ya alizeti, pia tunafungua ghala katika Jiji la Mombasa kwa ajili ya kuhudumia *processors* walioko katika nchi ya Kenya.

Mheshimiwa Spika, pia tumeanza juhudhi ya kuangalia uwezekano wa kufungua maghala katika nchi ya Kongo, especially Kongo Mashariki ili badala ya sisi kusubiri wanunuzi kuja katika nchi yetu tunahakikisha kwamba bidhaa zinakuwepo katika masoko yao na inakuwa rahisi kuwahudumia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jambo jingine la muda mrefu ni uwekezaji katika tija ili kupunguza gharama za uzalishaji na *cost per unit* na kufanya mazao yetu kuwa *competitive* katika masoko yanayotuzunguka. Moja ya soko kubwa ni nchi kama Kenya ambayo ina *deficit* ya zaidi ya tani laki sita kwa mwaka ya mahindi ambayo tunaichukulia kama ni fursa kubwa na kipato cha mwananchi wa Kenya asilimia 50 anatumia katika chakula.

Mheshimiwa Spika, hivyo, kwetu hili ni eneo la fursa na ndiyo maana tunaamua kuwekeza katika miundombini ambayo itatumika na Serikali lakini vilevile na sekte binafsi wanaweza kutumia kuuzia hizo *outlets* tunazofungua katika nchi hizo. (*Makofii*)

SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Neema Lugangira.

MHE. NEEMA K. LUGANGIRA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, hitaji la wakulima kuunganishwa na wawekezaji wa nje na ndani liliopo kule Mikoa ya Kusini linafanana kabisa na hitaji la wakulima wa zao la vanilla kutoka Wilaya za Bukoba, Misenyi, pamoja na Muleba Mkoani Kagera, ningependa kufahamu Serikali ina mpango gani wa kuunganisha wakulima wa zao la vanilla na wawekezaji wa kutoka nje na ndani ya nchi? Ahsante.

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Neema, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli zao la vanilla linalimwa katika Mkoa wa Kagera, vilevile ni moja kati ya zao linalokua katika Mkoa wa Kilimanjaro. Nikiri tu hapa kwamba miongoni mwa Wabunge ambao wamekuwa wakilifuatilia zao hili mmojawapo ni Mheshimiwa Neema na Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, Mbunge wa Mwanga - Kilimanjaro. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nataka tu niwahakikishie tumeanza mazungumzo na *local exporters* wa zao hili la vanilla ili tuanze kutengeneza mfumo wa *contract farming* moja kwa moja na mikataba. Mheshimiwa Shigongo naye ni mmoja kati ya waathirika wa zao hili, ili tuhakikishe zao hili linakua kwenye ramani, hili ni *high value commodity* na Wizara tumeanza kuwekeza kwenye *research and development*.

Kwa hiyo, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge ni zao jipya ambalo limeanza kuchukua nafasi na tunalitazama kwa ukaribu sana na kuwaunganisha na masoko. (*Makof*)

SPIKA: Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, swali la nyongeza.

MHE. SAASHISHA E. MAFUWE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo nami nilikuwa nauliza kuhusu vanilla, amenijibu vizuri mno na kutambua Wilaya yetu inalima zao hili.

Serikali kwa kuwa sasa imeona zao hili ambalo lina bei nzuri sana sokoni, mwanzoni ilikuwa ni 120,000 sasa hivi

limeshuka kwa sababu ya kukosa watu wa kuwaunganisha, kilo inauzwa 20,000.

Je, Serikali ina mkakati gani sasa wa kuhakikisha inatuletea wataalam sambamba na hili ambalo ametuambia la kutafutia masoko? Ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Kuhusu wataalam Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika Bunge lako Tukufu hili mlitupitishia ongezeko la bajeti ya Wizara ya Kilimo kwenye utafiti zaidi ya asilimia 90. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge moja ya eneo ambalo tunaenda kuwekeza sana ni kwenye utafiti na *training* ya Wataalam hasa wanaoshiriki katika shughuli za uzalishaji kwa maana ya Wagani.

Kwa hiyo, nimhakikishie kwamba, mwaka huu tunaanza *programya training* na Waziri wa kilimo wiki iliyopita amezindua *training* ya kwanza katika Wilaya ya Mpwapwa, Mkao wa Dodoma na zoezi hili linaendelea nchi nzima tutakuwa tuna-*train* kutokana na ikolojia na mazao husika ya eneo husika ya eneo husika ili kuwafanya wataalam waweze kufanana na mazao yaliyoko eneo hilo. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge tuendelee. Mheshimiwa Dkt. Pindi Chana kwa kuwa Njombe inakubali sana parachichi, timesikia hapa tani moja ni milioni moja na laki nane, kale ka-*pick up* kakijaa tu *it is a lot of money*. Sasa kwa nini mnang'ang'ania watu kuwaambia walime mahindi? Siyo *opportunity lost?* Watu wapande parachichi wapate hela.

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Issa Ali Mchungahela, Mbunge wa Lulindi. Mheshimiwa Mchungahela tafadhalii.

Hitaji la Kituo cha Uhamiaji Eneo la Chipingo

MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaweka Kituo cha Uhamiaji katika eneo la Chipingo ili kuondokana na vivuko bубу vilivyopo Mpakani mwa Tanzania na Msumbiji?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Mambo ya Ndani. Mheshimiwa Khamis Hamza Khamis, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, Mbunge wa Lulindi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Chipingo ni kipenyo kilichopo Wilaya ya Masasi katika mpaka wa Tanzania na Msumbiji kandokando ya Mto Ruvuma umbali wa Kilomita 86 kutoka Masasi Mjini. Kwa upande wa Msumbiji hakuna ofisi za Uhamiaji wala huduma za Uhamiaji bali kuna walinzi wa mpaka wa nchi hiyo.

Mheshimiwa Spika, ufunguaji wa vituo vya mipakani hutegemea makubaliano baina ya nchi zinazochangia mpaka. Kwa upande wa mpaka wa Tanzania na Msumbiji, kumebakii kituo kimoja cha mpakani kinachofanya kazi cha Mtambaswala kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo ghasia na hali tete ya usalama.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia maelezo hayo, Serikali inaendelea kufuatilia hali ya usalama katika mpaka huo na hali itakapotengemaa mawasiliano na Msumbiji yatafanyika ili kufungua vituo zaidi kuhudumia wananchi wanaotumia mpaka huo. Ninakushukuru.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Mchungahela.

MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA: Mheshimiwa Spika, hali ya kufunga mpaka huu kwa muda mrefu imesababisha mkwamo mkubwa wa kiuchumi kwa wananchi katika eneo hili.

Je, hivi Serikali haioni sababu ya kufungua mpaka huu kusudi wananchi wanufaikie na zile fursa zilizoko katika eneo lile? Ahsante.

SPIKA: Majibu ya swali hilo. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, Mbunge wa Lulindi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge kama ataangalia zaidi katika jibu langu la msingi nimesema kwamba, ufunguaji wa kituo hiki unategemea zaidi makubaliano ya nchi mbili baada ya kukaa na kuangalia namna ya kuweza kufungua kituo hiki kwa ajili ya kuwapatia huduma wananchi. Nimesema Serikali inaendelea kufuatilia hali hii ili kuona namna bora ya kuweza kukaa na jirani zetu, ili kuweza kuwafungulia.

Mheshimiwa Spika, kikubwa afahamu tu kwamba, lengo letu kubwa ni kuhakikisha kwamba wananchi wanapata huduma katika mpaka huu katika hatua za uingajji na utokaji na hali ya ulinzi na usalama inaendelea. Hivi tunavyozungumza viro vikosi vyetu ambavyo vinaweka amani na utulivu katika eneo hilo na huduma nyingine zinapatikana. Ninakushukuru.

SPIKA: Ahsante. Tunaendelea Wizara ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Neema William Mgaya, uliza swali lako tafadhalii.

Na. 116

Sababu za Kubadilisha Mfumo wa Ukaguzi wa Magari yanayotoka Nje

MHE. NEEMA W. MGAYA aliuliza: -

Serikali imewekeza kiasi cha Shilingi Bilioni 20 kwa ajili ya kutengeneza miundombinu ya ukaguzi wa magari nchini (*Destination Inspection*).

Je, ni sababu zipo zilisababisha Serikali kubadilisha mfumo huo?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Kigahe yupo? Ahsante, majibu tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Neema William Mgaya, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Shirika la Viwango Tanzania (*TBS*) lilianza kukagua magari yaliyotumika yanayoingia nchini kuanzia tarehe 01 Machi, 2021 katika Bandari ya Dar-Es-Salaam. Sababu za kusitisha utaratibu uliokuwepo awali (*Pre-Shipment Verification of Conformity to Standards – PVOCS*) ni pamoja na changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa mfumo huo na pia, faida tarajiba baada ya kutekeleza mfumo wa *Destination Inspection (DI)*.

Mheshimiwa Spika, changamoto za *PVOCS* ni pamoja na Mosi; ukosefu wa ufanisi, gharama kubwa za ukaguzi na upimaji. Mawakala kutokutokuwa na ofisi za ukaguzi katika maeneo yote, mawakala kushindwa kufanya ukaguzi inavyostahili, nchi kupoteza fedha za kigeni, upotevu wa ajira kwa Watanzania, nchi kushindwa kujenga uwezo wa miundombinu ya ukaguzi na wataalam wa ukaguzi na ugumu

wa kuhudumia Wajasiriamali Wadogo wanaonunua bidhaa nyingi za aina mbalimbali zenyenye thamani ndogo.

Mheshimiwa Spika, napenda kiliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, tangu ukaguzi huu uanze hapa nchini mwezi Machi hadi tarehe 25 Agosti, 2021 jumla ya magari 13,968 yamekaguliwa na *TBS* na kuliingizia Taifa jumla ya Shilingi 4,888,800,000 ikiwa ni tozo za ukaguzi. Aidha, wateja wengi wameridhika na kufurahia utaratibu huu wa *DI*. Nashukuru.

SPIKA: Mheshimiwa Neema nimekuona.

MHE. NEEMA W. MGAYA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, *Tanzania Bureau of Standards* na *Bureau of Standards* zote ulimwenguni kazi yake ni kulinda na kudhibiti ubora wa bidhaa zinazoingia nchini na zinazozalishwa ndani ya nchi.

Je, utakubaliana nami kwamba, *TBS* haipimwi kwa kiasi cha pesa inazoingiza nchini, kutokana na jibu lako ulilonijibu katika swali langu la msingi?

Swali la pili; kuna wale ambao wanashindwa kulipia yale magari, kwa kushindwa huko kulipia yale magari inabidi yale magari mtueleze mnapeleka wapi yale magari? Hamuoni kwamba, *Tanzania* mnataka kuigeuza kuwa *dumping area?* (*Makof!*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo mawili Mheshimiwa Naibu Waziri Viwanda na Biashara, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Neema Mgaya, Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Neema kwa ufuatiliaji wa siku nyingi kuhusiana na ubora wa bidhaa zinazoingizwa nchini. Ni kweli, kazi ya msingi ya *TBS* ni kuhakikisha na kudhibiti ubora wa bidhaa zote zinazoingizwa

nchini ndiyo maana tumeamua sasa ili kuwa na ufanisi katika hilo kukagua sisi wenyewe kwa sababu kama nilivyosema katika jibu la msingi, baadhi ya mawakala huko nje walikuwa hawafanyi kazi ipasavyo na malalamiko bado yalikuwa mengi sana kwamba kuna baadhi walikuwa wanaletewa bidhaa ambazo hazina ubora lakini kwa sababu tayari mawakala walikuwa wamethibitisha kwa hiyo maana yake *TBS* ilikuwa haina namna ya kufanya.

Mheshimiwa Spika, Iakini kwa sababu sasahivi tunathibitisha wenyewe, pia tumeshawaambia makampuni yanayoleta bidhaa nchini kuhakikisha wanaleta bidhaa ambazo zina ubora. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Neema kwamba kazi hiyo inafanyika na ndiyo maana tunaamua kujiimarisha sasa ili *TBS* waweze kufanya kazi hiyo kwa uthabiti.

Mheshimiwa Spika, pili, kuhusu ubovu wa bidhaa au magari yaliyotumika yanayoingizwa nchini, kama nilivyosema mpaka sasa zaidi ya wateja hao 13,968 ambaao wameingiza magari nchini hakuna hata mteja mmoja ambaye amelalamika kuhusiana na ubovu wa magari au bidhaa zinazoingizwa. Kwa hiyo, tunaamini sasa mfumo huo utaenda kuboreshwa zaidi kwa maana ya kukagua kwa ubora zaidi na tunawaelekeza wateja wetu kuhakikisha wanaingiza bidhaa kupitia makampuni ambayo tumekubaliana ambayo yanatoa bidhaa hizo kutoka nje. Ninakushukuru.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Zaytun Swai, bado tuko Viwanda na Biashara.

Na. 117

Malipo kwa Wafanyakazi wa Kiwanda cha Kiliflora – Meru

MHE. ZAYTUN S. SWAI aliuliza: -

Je, ni lini akina Mama zaidi ya 300 waliokuwa Wafanyakazi wa Kiwanda cha Kiliflora Wilayani Meru watalipwa stahiki zao baada ya Kiwanda hicho kufungwa?

SPIKA: Bado tuko kwako Mheshimiwa Silaoneka Kigahe, Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, naomba kujibu swali la Zaytun Seif Swai, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua mgogoro uliopo baina ya wafanyakazi na mwekezaji wa Kampuni ya Kiliflora Ltd. Hivyo, Serikali ilifuatilia mgogoro huo na kubaini kuwa *Tanzania Investment Bank (TIB)* ilirejesha fedha iliyokopesha kwa kuuza mali za Kiliflora *Ltd* zilizowekwa dhamana ili kulipa deni la mkopo uliochukuliwa na Kampuni. Hivyo, kisheria Wafanyakazi wanapaswa kulipwa na Kampuni ya Kiliflora kwa kuwa kilichofanyika ni ufilisi kabidhi na siyo kufunga kampuni. Mfilisi Kabidhi (*Receiver and Manager*) ni tofauti na Mfunga Kampuni (*Liquidator*).

Mheshimiwa Spika, aidha, wafanyakazi wa Kiliflora *Ltd*, Wilson Samwel na Wenzake 502 walifungua Kesi ya *LaborNa*. ARS/ARM/305/2020, 152/2020 dhidi ya Kampuni ya Kiliflora *Ltd* na Frank Mwalongo ambaye ni Mfilisi Kabidhi ambayo ilianza kusikilizwa tarehe 30/10/2020. Shauri hili lilikwishatolewa maamuzi na Mahakama kwamba, masuala ya madai ya wafanyakazi yanapaswa kufanyiwa kazi na Kampuni ya Kiliflora *Ltd* maana haijafilisiwa kama ilivyonekana kwenye taarifa za *BRELA* kwamba, Kampuni bado ipo hai.

Mheshimiwa Spika, Serikali kuitia Wizara ya Fedha na Mipango inaendelea kuhimiza mmiliki wa shamba la Kiliflora kuwalipa akina mama hao. Nakushukuru.

SPIKA: Mheshimiwa Zaytun Swai.

MHE. ZAYTUN S. SWAI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Naibu Waziri, sijaridhika na majibu yake. Kwa taarifa rasmi zilizopo ni

kwamba, viwanda hivi pamoja na mashamba viko chini ya Msajili wa Hazina. Msajili wa Hazina pamoja na Wizara ya Fedha ndiyo wanaotakiwa kuwalipa wafanyakazi hawa.

Mheshimiwa Spika, naomba kusikia *commitment* ya Serikali. Je, ni lini wafanyakazi hawa 502 watalipwa na Serikali? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; Viwanda hivi vinaenda sambamba na mashamba yale maua na mbogamboga. Mashamba haya na viwanda ni muhimu sana kwa uchumi wa wananchi wa Mkoa wa Arusha pamoja na sekta hii ya maua na mbogamboga.

Naomba kujua Serikali ina mikakati gani wa kuyafufua mashamba haya? Ahsante. (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya maswali haya, Mheshimiwa Naibu Waziri Fedha. *Engineer Masauni*, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, napenda kuongezea majibu mazuri ambayo amejibiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, siyo sahihi kwamba Serikali ndiyo inapaswa kulipa madeni haya, kwa sababu kama ambavyo ameeleza Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda kwamba *TIB* ilipewa dhamana ya kuhakikisha kwamba inarudisha fedha ambazo Kiliflora ilikuwa imekopeshwa. Fedha hii ilirudishwa kupitia mnada ambapo Serikali ilinunua mashamba yale kihalali, lakini hawa ambao wanadai wanadai vitu viwili vikubwa: Kwanza wanadai malimbikizo ya mishahara kwa kampuni ambayo ilikuwa imewaaajiri pamoja na mafao.

Mheshimiwa Spika, haya ni madai ambayo yanapaswa kulipwa na mwajiri ndiyo maana hata katika kesi waliyofungua walimshitaki muajiri na Mahakama kupitia Tume

ya Usuluhishi wakatoa maamuzi kwamba, hii kampuni iwalipe kwa hiyo, maamuzi tayari yalishatoka kwamba, kampuni hii ndiyo inapaswa kuwalipa hawa wadai.

Mheshimiwa Spika, nawashauri hawa wadai kwamba pengine wangeweza kuwasiliana na vyombo nya dola ili waweze kuwasaidia kuwatafuta hawa wanaowadai waweze kuwalipa mali yao.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na namna ambavyo mashamba haya yataendeleza kwa sababu, mashamba haya sasa hivi yapo tayari kwa Serikali, kuna mikakati mikubwa ya kuhakikisha kwamba tunaimarisha sekta ya kilimo kupitia rasilimali mbalimbali ambazo zinamilikiwa na Serikali, yakiwepo mashamba haya, lakini kwa kuwa, sasa hivi muda ni mfupi siwezi kueleza mikakati hiyo ambayo iko chini ya benki ya *TIB* kwa kirefu.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo Mheshimiwa Mbunge nitakupatia baadae. (*Makof*)

SPIKA: Tunaendelea na Wizara ya Fedha na Mipango. Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo uliza swali lako.

Na. 118

Hatma ya Maduka ya Kubadilishia Fedha Nchini

MHE. PRISCUS J. TARIMO aliluliza:-

Je, ni nini hatma ya biashara ya maduka ya kubadilisha fedha (*Bureau de Change*) yaliyofungwa na Serikali?

SPIKA: Majibu ya swali hili muhimu. Mheshimiwa Naibu Waziri Fedha, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, Mbunge wa Moshi Vijijiini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ukaguzi ambao umefanyika mwaka 2018/2019 ulisababisha maduka mengi ya kubadilisha fedha za kigeni kufungwa kutokana na kubainika kuendesha biashara bila kuzingatia sheria na kanuni husika. Baada ya kufungwa kwa maduka hayo, benki za biashara nchini zilihamasishwa kuendelea kutoa huduma ya kubadilisha fedha za kigeni katika matawi yake yote nchini. Kwa sasa benki zote za biashara zinatoa huduma hizo nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, pia maduka ambayo hayakufungwa yameendelea kufungua matawi na kutoa huduma hizo katika miji mbalimbali nchini. Kwa ujumla hali ya upatikanaji wa huduma ya kubadilisha fedha za kigeni nchini ni ya kuridhisha. Aidha, maduka yaliyofungwa pamoja na kampuni nyingi ambayo yanayotaka kufanya biashara ya kubadilisha fedha za kigeni nchini, yanaruhusiwa kuomba leseni Benki Kuu kwa kuzingatia matakwa ya Sheria za Fedha za Kigeni ya mwaka 1992 pamoja na Kanuni za Biashara ya Kubadilisha Fedha za Kigeni ya mwaka 2019. Hadi kufikia tarehe 30 Julai 2021, Benki Kuu ilikuwa imepokea maombi mapya manne ya leseni ya biashara ya kubadilisha fedha za kigeni ambazo yanafanyiwa uchambuzi na watusika watapewa leseni iwapo watakuwa wamekidhi vigezo.

SPIKA: Mheshimiwa Priscus.

MHE. PRISCUS J. TARIMO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyogezo.

Kwa kuwa vigezo vipyta vyta kufungua maduka vimekuwa vigumu kwa wafanyabiashara wengi, ikiwa ni pamoja na uoga wa kupoteza fedha kama ilivyo tokea mwanzo, Serikali ina mpango gani wa kuweka masharti ambayo ni rafiki ili wafanyabiashara wengi zaidi wafungue biashara hizo kwa sababu maeneo ya mpakani/mikoa hii ya

mpakani kumeshaanza kuwepo kwa *black market* ambapo wale wanaobadilisha fedha wanabadilisha kwa bei ya chini sana? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, swalii la pili; maduka yale yaliyofungwa fedha taslimu zilichukuliwa na baadhi ya wafanyabiashara zilichukuliwa mali zao nyngi ikiwepo hati za viwanja na nyumba, hati za magari kwa maana ya kadi za magari na hawajarejeshewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni nini hatma ya watu hawa ambao wamefungwa mikono na mali zao zimeshikiliwa na Serikali? (*Makof*)

SPIKA: Majibu ya swalii hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Fedha na Mipango tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Tarimo Mbunge wa Moshi Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge amesema kwamba vigezo viliviyowekwa ni vigumu, lakini bahati mbaya hakuainisha vigezo hivyo ni vipi vigumu; kwasababu imani yangu ni kwamba pengine angetusaidia kutuambia ni kipi kigumu tungeweza kukifanya kazi. Hata hivyo kwa ujumla vigezo viliviyowekwa mpaka sasa hivi tunadhani tumeviwekwa kwa kuzingatia maslahi ya nchi pamoja na maslahi ya Serikali. Ingawa bado kuna mwanya wa kuweza kuiyangalia kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge amesema, lakini kwa uelewa wangu vigezo hivyo kwa kweli si vingi sana. Labda kigezo kimoja ambacho kimekuwa kikilalamikiwa sana ni kigezo cha kiwango cha mtaji kutoka shilingi milioni 300 kuja bilioni moja.

Mheshimiwa Spika, mantiki ya kuweka kigezo hiki ilikuwa ni nia njema tu ya Serikali kuhakikisha kwamba hawa wafanyabiashara wa maduka haya ya kubadilisha fedha wanatumia fedha zao wenyewe kuendesha biashara. Kwasababu wakati ambapo umefanyika utafiti kuititia

forensic audit iliyo fanywa iligundulika kwamba wengi wafayabiashara wa biashara hizi za kigeni walikuwa wanazungusha fedha isiyokuwa yao, kwa hiyo, hiyo ndio ikawa mantiki ya kuweka kiwango hicho na hivyo nadhani ndio malalamiko mengi makubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Mheshimiwa Mbuge labda pengine angetusaidia kwa wakati wake kuweza kuainisha vigezo. Kama kuna vigezo ambavyo tunaona kwamba vinahitaji kuangaliwa basi tutaviangalia.

Mheshimiwa Spika, lakini swali lake lingine ambalo ameuliza anazungumzia kuhusiana na hatma ya vifaa vilivyo chukuliwa. Ni kwamba baada ya hatua ambazo zimechukuliwa kujitokeza wafanyabiashara hawa waliitwa ili kufanya majadiliano na mamlaka husika; na baada ya majadilliano kumalizika walitakiwa wale ambao walipaswa kulipa walipe, wale ambao walitakiwa kwenda kuchukua vifaa vyao waende wakavichukue.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nitoe wito, kama kuna wafanyabiashara ambao bado hawajachukua vifaa vyao na wanastahili kwenda kuvichukua vifaa vyao waende wakachukue vifaa vyao, na hakuna sababu yoyote ambayo Serikali inaweza kukaa na mali ya mtu bila sababu ya msingi. Kwa hiyo niendelee kuwasistiza kwamba kauli rasmi ya Serikali ni kwamba kama ambavyo majadiliano yalifanyika wakaelezwa wale ambao wanastahili kwenda kuchukua au wanahitaji kuvichukua basi waende wakavichukue. Kama kuna mapungufu yoyote basi tuletewe hizo taarifa ili tuweze kuzifanyika kazi.

SPIKA: Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda nimekuona, Mheshimiwa Ole-Sendeka atamalizia.

MHE. KILUMBE S. NG'ENDA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, nilitaka kujuua kama Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Benki Kuu waliamua kufunga maduka

ya fedha za kigeni kwa sababu yalikuwa hayafuati taratibu, na sasa zipo *financial institution* nydingi mjini humu ambazo zinakopesha kwa riba ya juu na kuumiza walimu na watumishi wengine wa umma. Hivi Serikali inapata kigugumizi gani kuzifunga hizi ambazo zinatesa wananchi na badala yake inakwenda kufunga maduka ya fedha za kigeni ambayo yalikuwa hayalalamikiwi na wananchi?

SPIKA: Majibu ya swali hili muhimu sana taasisi zinanyonya sana watu hizi, Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda, Mbunge wa Kigoma Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kilichofanyika ilikuwa ni kuzifuta leseni kwa wale ambao walibainika kuwa wamekiuka taratibu; na hii ipo kwa mujibu wa sheria pamoja na *regulation* ambazo tumetunga za mabadiliko ya fedha za kigeni, wanaita *Foreign Exchange Act*, kwa hiyo hii ilichofanyika imefanyika kwa mujibu wa sheria.

Sasa kuhusiana na kwamba kwanini kuna taasisi nydingine ambazo zinaumiza wananchi wa riba kubwa, jana nilimpongeza sana Mheshimiwa Kilumbe hapa, kwasababu nilisema kwamba kama kuna Wabunge ambazo walishiriki katika mjadala wa Bunge la Bajeti liliopita, kuzungumza kwa uchungu na hisia kazi juu ya baadhi ya taasisi ambazo zimekuwa zikinyanyasa wananchi kwa kuwakopesha kwa riba kubwa bila msingi yeye alikuwa ni mmojawapo. Nikasema kwamba kwa kusikia kilio hicho hicho kwa Waheshimiwa Wabunge Mheshimiwa hakuchelewa kwa kutoa maelezo ili jambo hilo lifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Spika, na nimewahakikisha juzi na jana wakati najibu maswali kwamba kwanza niwapongeze *BOT* kwa kutekeleza maelekezo ya Mheshimiwa Rais, sasa hivi mchakato huu umeshaanza. Kwa hiyo ni matarajio yangu sasa kile kilio cha Waheshimiwa Wabunge akiwepo

Mheshimiwa Kilumbe cha kupunguza riba sasa kimepatiwa dawa. Kwa hiyo hoja hizo mbili zote zinachukuliwa hatua kwa utaratibu wake kulingana na sheria na taratibu za nchi yetu.

SPIKA: Mheshimiwa Ole-Sendeka ulikuwa umesimama.

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Serikali ya Awamu ya Sita imetangaza nia yake ya kuendelea kurejesha imani ya wafanyabiashara na kujenga mahusiano mazuri kati ya Serikali na wafanyabiashara. Na kwa kuwa sasa hivi Serikali inaendelea kujadiliana na watu hawa wa maduka ya kubadilisha fedha.

Je, Serikali itakuwa tayari kuweka bayana kiasi cha fedha kilichokusanya wakati wa *operation* hiyo, na kiasi cha fedha ambazo zitakuwa zimerudishwa kwa wale wasio na hatia na sababu zitakazopelekea wale ambao fedha zao zitachukuliwa na kwamba zitakuwa zimechukuliwa kwa misingi ipi? Naliweka hili na naomba swali langu ijibowi. (*Makof!*)

SPIKA: Majibu wa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Fedha na Mipango tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ole-Sendeka, Mbunge wa Simanjiro kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni sahihi kabisa, Serikali ya Awamu ya Sita imedhamiria sana kuhakikisha kwamba imani ya wafanyabiashara inaimarika Zaidi. Na kama ambavyo Mheshimiwa Rais mwenyewe amekuwa akisema kwamba Serikali yake itahakikisha kwamba itafanya kila linalowezekana kuhakikisha inaibia vyanzo vya mapato. Jtihada mbalimbali mmeshaziona ambazo Mheshimiwa Rais mwenyewe binafsi amezifanya katika kuhakikisha kwamba

anahamasisha uwekezaji nchini ili tuweze kupata wawekezaji wengi wakubwa waweze kutupatia kodi katika nchi hii; na amesema mara kadhaa kwamba hataki kuona kodi ya dhuluma.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Wizara ya Fedha na Mipango tutakuwa watu wa mwisho sana kuona kwamba kama kuna mwananchi yejote anadhumumiwa kuititia utaratibu wa kodi na tukalifumbia macho jambo hilo.

Kwa hiyo, niwahakikishie tu kwamba katika hoja hii hawa ambao wanahusiana na maduka ya fedha za kigeni tumefuatilia kwa kina na tumebaini kulingana na taarifa ambazo tunazo na vielelezo kadhaa ambavyo tunavyo, kwamba walihusishwa wenyewe mara kadhaa katika mchakato mzima wa mgogoro uliojitokeza. Imani yetu ni kwamba kama nilivyzungumza, kwamba wengi wao wamekubaliana na hali halisi baada ya kupewa ushahidi juu ya matukio mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, lakin kama kuna wale mnadhani bado, basi bado nafasi hiyo ipo kwa sababu Serikali hii imetoa mwanya na nafasi kwa yejote ambaye anadhanani bado hajatendewa haki kuweza kufuata taratibu za kudai haki yake ili aweze kuipata.

SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Mbunge wa Arusha Mjini swali la mwisho eneo hili.

MHE. MRISHO M. GAMBO: Mheshimiwa Spika, kwa sababu kumekuwa na malalamiko mengi sana kwa wafanyabiashara wa *bureau*, kwamba *assessment* ambazo zimefanyika hazikufanya na *competent authority* kwa sababu zilifanya na *task force* badala ya kufanya na *TRA* kama wahusika.

Je, Wizara ya Fedha haioni sasa kwamba wakati umefika kwa *TRA* kwenda kuititia upya zile *assessment* ili yale makadirio yaani makadirio ambayo yapo kwa mujibu wa sheria?

Mheshimiwa Spika, lakini la mwisho ...

SPIKA: Hauruhusiwi ni moja tu la nyongeza.

MHE. MRISHO M. GAMBO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri ufanuzi wa jambo hilo.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Mrisho Gambo Mbunge wa Arusha Mjini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ninatambua Mheshimiwa Mrisho Gambo ni miongoni mwa watu ambao wananchi wa jimboni kwake wameathirika na jambo hili; na ikiwa kama Mbunge anawajibu anapopelekewa malalamiko na wananchi hapa ndipo sehemu yake pa kuyasemea.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo nimhakikishie Mheshimiwa Gambo kwamba *assessment* hii imefanywa na *TRA* kuititia Kitengo kile cha *Investigation*, kwa hiyo ni *assessment* ambayo imefanywa kwa mujibu wa taratibu na sheria na mamlaka sahihi kabisa ambayo inapaswa kufanya *assessment*.

Mheshimiwa Spika, lakini kama nilivyosema mwanzo, kwamba tuna utaratibu ambao iwapo mtu hajaridhika na *assessment* yote kuna utaratibu wa kufuata ili kuweza kuhakikisha kwamba anakata rufaa katika ngazi mbalimbali na kuangalia kama kuna uwezekano wa kuweza kui-review *assessment* yake ukafanyika hivyo.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie tu kwamba jambo hili lili simamiwa na *TRA* wenyewe katika eneo la *investigation*.

SPIKA: Ahsante sana. Swalii la mwisho kwa siku ya leo Mheshimiwa David Kihenzile.

Na. 119

Kupunguza kodi Vifaa vya Michezo

MHE. DAVID M. KIHENZILE aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kupunguza Kodi kwenye Vifaa vya Mchezo ili Sekta ya Michezo iweze kustawi.

SPIKA: Majibu ya swali hilo bado tupo kwako Fedha na Mipango Mheshimiwa Eng. Masauni tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa David Mwakaposa Kihenzile, Mbunge wa Mufindi Kusini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali kwa kuona umuhimu wa Sekta ya Michezo nchini, imetoea msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye nyasi bandia kwa viwanja vya mpira viliviyopo kwenye Manispaa na Majiji.

Aidha, Serikali itaendelea kutoa msamaha wa VAT kwenye nyasi bandia kwa viwanja vya mpira viliviyopo kwenye Halmashauri baada ya kuridhishwa na matumizi ya msamaha uliotolewa kwenye Manispaa na Majiji. Aidha, katika kuendeleza Sekta ya michezo nchini Serikali imetoea msamaha wa VAT kwenye huduma za elimu zitolewazo kwenye vituo vya mafunzo ya michezo nchini.

SPIKA: Mheshimiwa Kihenzile nimekuona.

MHE. DAVID M. KIHENZILE: Mheshimiwa Spika, sote tunafahamu dhamira ya Rais wetu alioioneshwa kwenye eneo la michezo, na tarehe 15 Juni, 2021 alipokuwa anazungumza na vijana wa nchi hii pale Mwanza alizungumzia eneo hili la msamaha wa kodi. Na katika maelezo ya Mheshimiwa Naibu

Waziri amesema wataanza kufanya *practice* kwenye upande wa majiji na halmashauri za manispaa, na wakifanya vizuri watahamia kwenye Wilaya.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; ina maana wanamaanisha kwa mfano kama Dodoma Mjini wakipewa hayo majoribio waki *under perform* basi ina maana Kongwa hawatapewa kwenye phase two.

Mheshimiwa Spika, hii nadhani si sawa. Ni vyema kama wanakwenda kufanya majoribio wafanye kote kwenye halmashauri za manispaa, majiji na kule kwingine.

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Ili kurahisisha utekelezaji wa jambo hili Je, Mheshimiwa Naibu Waziri na Serikali kwa ujumla haioni sasa umefika wakati wa kuanzisha wakala wa vifaa vya michezo nchini ili kurahisisha upatikanaji wa vifaa vya michezo kirahisi kuanzia kwenye shule zetu hata kwa Wabunge wenyewe ambao kimsingi kila mwaka wamekuwa wakiagiza vifaa vya michezo kwa wananchi wao? (*Makofii*)

SPIKA: Majibu wa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mwakiposa Mbunge wa Mufindi Kusini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, dhamira ya Serikali kuanza na majiji na halmashauri hayakuwa na maana ya kuangalia mapungufu ambayo yanaweza kusababisha maeneo mengine yasipate sipokuwa yalikuwa yana lengo la kuangalia mapungufu ili yatakapopelekwa maeneo mengine mapungufu yale yasijitokeze. Kwa mfano katika matumizi ya nyasi hizi bandia yamekuwa yakitumika katika shughuli mbalimbali wakati mwингine unaweza ukaenda hata kwenye *barukakuta* hizi nyasi bandia zipo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nikuhakikishie kwamba Serikali inadhibiti matumizi mabaya ya fursa hii njema

iliyowekwa na kwa dhamira njema ya Serikali ni vyema tunganeza hatua kwa kwa hatua. Kwa hiyo elimu ambayo tumepata katika utekelezaji katika awamu ya halmashauri na majiji itatusaidia tunapopanua wigo katika maeneo mengine mengi zaidi kuweza kufahamu ni mapungufu yapi na tukayoweza kuyadhibiti kirahisi ili kuepuka madhara na hasara kwa Serikali; hiyo ndiyo iliyokuwa dhamira. Malengo ni kuhakikisha kwamba tunasambaza huduma hizi katika maeneo yote nchini hatua kwa hatua na awamu kwa awamu.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na wazo lake la pili, ni jambo jema sana na Mheshimiwa Mwakiposa amekuwa kwakweli ni mpambanaji sana wa suala hili. Mara nydingi amekuwa akija akituulizia kuhusiana na utekelezaji, na kwamba angependa kuona mabadiliko na maboresho makubwa katika eneo hilli. Kwa hiyo kuhusiana na hoja hili ya pili nadhani ni hoja ya msingi. Mheshimiwa Waziri wa Michezo na Mheshimiwa Naibu wake hapa wapo, wamesikia na ninahakika watalitafakari na kama wataona kuna tija basi watalitekeleza. Hili lipo katika Wizara ya Michezo na Serikali hapa ipo, tumelisikia.

SPIKA: Makamu wa Mwenyekiti wa Bunge *sports Club* swali la mwisho kabisa kabisa kabisa.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa michezo ni afya na kwa sasa dunia nzima ikiwemo Tanzania tunakabiliwa na hili janga la corona na hivyo tunawahamasisha wananchi wetu waweze kufanya mazoezi ikiwepo kushiriki michezo na vifaa vya michezo ni ghali sana. Na kwa kuwa michezo ni ajira kama Taifa tunahitaji kuwekeza kwenye michezo kuanzia kwenye makuzi ya awali ya watoto wetu ili baadaye waje kuwa na vipaji mbalimbali kwenye soka, riadha, *basket* na mengine; lakini zaidi michezo ni moja ya sekta ambayo inatangaza nchi yetu na kutangaza utalii. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, je, Serikali haioni kwamba ni vyema sasa iweze kufanya *exemption* kwa vifaa vyote vya

michezo ili viweze kuwa na bei nafuu na watanzania wengi waweze kununua na kujiedeleza kimichezo?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, *exemption* ya vifaa hivyo vya michezo.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Esther Matiko Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, suala la *exemption* si jambo ambalo linaweza likatolewa kauli Bungeni, linahitaji mambo mengi ikiwemo uchambuzi wa kina wa kitaalam juu ya faida na hasara zake. Sisemi kwamba vifaa vya michezo havina faida lakini ni jambo ambalo siwezi ukalizungumza hapa. Niseme tu kwamba tumelichukua tuone jinsi gani litakavyokuwa linakidhi mahitaji na vigezo kwa wakati husika basi tutalifanyi kazi.

SPIKA: Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge, tulikuwa tunamalizia dawati letu kuhakikisha kwamba tunapoondoka hatuna swali hata moja lilllobakia katika yale yaliyopangwa katika Mkutano huu wa nne, ahsanteni sana. Sasa Wageni waliopo Bungeni jioni hii ni wageni nane wa Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson - Naibu Spika ambao ni pamoja na *Program Manager* wa *Msichana Initiative*, Ndugu Consolata Chikoti; karibu sana Consolata. Pia yupo *Program Specialist UN Woman* - Rachael Boma; karibu sana Rachael. Yupo *Executive Director* wa *TAMWA* - Dkt. Rose Reuben, ahsante. (*Makofii*)

Yupo *Board Member* wa *WFT*, Dkt. Dinah Richard Mbaga, karibu sana; yuko *Coordinator - Tanzania Ending Child Marriages Network* Ndugu Euphomia Edward, ahsante; yupo *Program Officer* wa *Msichana Initiative* - Ndugu Lucy Gidamis, ahsante sana; yupo *Program Officer Msichana Initiative* - Ndugu Mgusuh Maswi, ahsante sana; yupo *Board Member* wa *Tanzania Youth Vision Association* Ndugu Nuriah Mshare, karibuni sana. (*Makofii*)

Baada ya hapo, ninayo baadhi ya matangazo kabla hatujaendelea na shughuli inayofuata; Naibu Waziri Maliasili na Utalii anawatangazia Waheshimiwa Wabunge na kuitia ninyi Watanzania wote kwamba kuna maandalizi makubwa kwa ajili ya wenye nia ya kupanda Mlima Kilimanjaro kati ya tarehe 19 na tarehe 25. Kwa yeote anayetamani kupanda Mlima Kilimanjaro atakuwa anaunga mkono juhudzi za Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan katika kutangaza vivutio vyetu na kwa hiyo mnakaribishwa kuwasiliana naye Mheshimiwa Naibu Waziri, zoezi ni kuanzia tarehe 19 hadi 25 mwezi huu. Mambo haya yanataka ubavu, siyo una vichomi vichomi halafu hata hatua 20 hazifiki simu inapigwa Dodoma kwa Spika kwamba lete helkopta huku. (*Makofi/Kicheko*)

Katibu wa Bunge anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge kwamba Ofisi imegawa nakala za Jarida la Bunge, Toleo la Julai, 2021 kwa Waheshimiwa Wabunge wote. Jarida hili limeangazia matukio mbalimbali yaliyotokea kuanzia kipindi cha Kamati mwezi Machi hadi Mkuano wa Tatu wa Bunge la Bajeti ulipoahirishwa tarehe 30 Juni 2021. Aidha, Jarida limebeba makala elimishi kuhusu masuala ya Kibunge. Ni jarida zuri ni vizuri kulichukua na kuitia na kuona baadhi ya kumbukumbu ya mambo ambayo yamekuwa yakiendelea Bungeni na unaweza ukalitunza kwa miaka mingi likakukumbusha wakati huo *what happened*. Jarida hili ni endelevu na litakuwa linatolewa mara tatu kwa mwaka. Nampongeza Katibu wa Bunge na Sekretarieti yake kwa hatua hii kubwa ya ubunifu, ahsante sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, hivi karibuni kumekuwa na barua kutoka Ofisi ya Bunge iliyotafsiriwa kuwa inawazuia Waheshimiwa Wabunge kuambatana na wenza wao au wasindikizaji wao kwenye ukumbi wa watu mashuhuri (*VIP*) kwenye Uwanja wa Ndege wa JK Nyerere. Waheshimiwa Wabunge wanayo haki ya kutumia huduma za ukumbi wa *VIP* kwenye viwanja vya ndege hapa nchini. Aidha, Ofisi ya Bunge inawajibika kugharamia huduma za viburudisho kwa Waheshimiwa Wabunge tu. Hapa tuelewane, Ofisi ya Bunge inawajibika kugharamia huduma za viburudisho tu kwa

Waheshimiwa Wabunge siyo unaenda pale unaagiza *larger kubwa, castle.* (*Kicheko/Makofi*)

Kwa hiyo, ni kwa Wabunge tu na siyo wenza wao au wasindikizaji. Pale Mheshimiwa Mbunge anapoambatana na mwenza wake au msindikizaji itabidi amilipie yeye mwenyewe. Nadhani tumeelewana, tunaomba mzingatia maelekezo hayo.

Waheshimiwa Wabunge, naomba niwape taarifa kwamba katika Kikao cha 62 cha Mkutano wa Tatu wa Bunge, Bunge lilipitisha Muswada uitwao Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na.3 wa Mwaka 2021 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendment) (No.3), Bill 2021*].

Napenda kuliarifu Bunge hili Tukufu kwamba tayari Muswada huo umekwishapata kibali cha Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuwa sheria ya nchi. Sasa ni sheria ya nchi iitwayo Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 2), Sheria Na. 4 ya Mwaka 2021 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendment) (No.2), Act No.4 of 2021*].

Baada ya matangazo haya, sasa tuendelee, Katibu.

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:

TAARIFA YA KATIBU WA BUNGE

NDG. NENELWA MWIHAMBI, ndc - KATIBU WA BUNGE:

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 35(2) ya Kanuni za Bunge, naomba kutoa taarifa kwamba shughuli zote zilizopangwa kwa ajili ya Mkutano wa Nne wa Bunge sasa zimemalizika.

SPIKA: Katibu tena.

NDG. NENELWA MWIHAMBI, ndc - KATIBU WA BUNGE:

HOJA YA KUAHIRISHA BUNGE

SPIKA: Hoja ya Kuahirisha Bunge, sasa naomba nimuite mtoa hoja hiyo na si mwine bali ni Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa. Mheshimiwa Waziri Mkuu, karibu tafadhalii. (*Makofi*)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Leo hii tunafikia tamati ya Mkutano wa Nne wa Bunge la Kumi na Mbili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ulioanza kikao chake cha kwanza tarehe 31 Agosti, 2021. Hivyo, hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu mwangi wa rehema kwa kutuwezesha kuhitimisha shughuli zote zilizopangwa kwenye mkutano huu tukiwa buheri wa afya.

Mheshimiwa Spika, vilevile, nakushukuru wewe binafsi kwa kumudu kullongoza vema Bunge hilli Tukufu, ukisaidiwa na Mheshimiwa Naibu Spika kwa pamoja na Waheshimiwa Wenyevitii wa Bunge. Aidha, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango mizuri mliyoitoa kwa kusema na kwa maandishi vilevile kwa kuchangia hoja mbalimbali zilizowasilishwa na Serikali kwenye mkutano huu. Nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuwa, Serikali kwa upande wake iko tayari muda wote kupokea michango yenu yenye lengo la kusaidia kuboresha utekelezaji wa mipango yake.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa Salamu za pole, niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kukupa pole kufuatia taarifa za kuhuzunisha za kifo cha Mheshimiwa Elias John Kwandikwa aliyejewa Mbunge wa Ushetu na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kilichotokea tarehe 2 Agosti, 2021. Aidha, natoa pole kwa familia ya marehemu, ndugu, jamaa, marafiki na wananchi wote wa Jimbo la Ushetu kwa kuondokewa na mwakilishi wao huyo.

Mheshimiwa Spika, vilevile, natoa salamu za pole kwa Kamanda Simon Nyakoro Siro, Inspekte Jenerali wa Polisi kufuatia tukio lililotokea tarehe 25 Agosti, 2021 Jijini Dar es Salaam, ambapo askari wetu wazalendo wapatao watatu

na mlinzi mmoja wa kampuni binafsi waliuawa wakati wakitekeleza majukumu yao ya kiusalama. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi na awape uponyaji wa haraka majeruhi wote waliookea katika tukio hilo. Amin!

Mheshimiwa Spika, nitumie pia nafasi hii kuwapa pole Watanzania wenzangu walipoteza ndugu, jamaa na marafiki na wengine kupata ulemavu katika matukio mbalimbali ikiwemo ajali za barabaranî zilizogharimu maisha ya maafisa watano wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*), waliofariki dunia tarehe 23 Agosti, 2021 wakati wakitekeleza majukumu yao ya kikazi mkoani Songwe. Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahala pema peponi, Amina!

Mheshimiwa Spika, Shughuli za Bunge. Wakati wa Mkutano huu wa Nne wa Bunge la Kumi na Mbili, Waheshimiwa Wabunge wamepata fursa ya kuuliza maswali ya msingi 119 na maswali 225 ya nyongeza ambayo yalijibowi na Serikali. Kadhalika, maswali 14 ya papo kwa papo yaliulizwa na Waheshimiwa Wabunge na kujibiwa na Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Waheshimiwa Wabunge walijadili na kuitisha Maazimio Mawili ya Bunge: Azimio la Bunge kuhusu kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Viwango vya Afya ya Mimea, Wanyama na Usalama wa Chakula (*East African Community Protocol on Sanitary and Phytosanitary – SPS Measures*); na Azimio la Bunge kuhusu kuridhia Mkataba wa Uanzishwaji wa Eneo Huru la Biashara la Afrika (*African Continental Free Trade Area*).

Mheshimiwa Spika, kuridhiwa kwa Maazimio haya kutasaidia nchi yetu kuimarisha biashara na uwekezaji kwenye ukanda huu wa Afrika Mashariki sambamba na kuongeza shughuli za biashara na uwekezaji wa ndani baina ya nchi wanachama wa Umoja wa Afrika. Kadhalika, kutaiwezesha Tanzania kuimarisha ushirikiano na mataifa mengine wanachama wa Umoja wa Afrika.

Mheshimiwa Spika, Miswada ya Sheria. Waheshimiwa Wabunge pia walijadili na kupitisha Miswada mitano ya Sheria iliyowasilishwa na Serikali katika mkutano huu kama ifuatavyo: -

(i) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 2 wa Mwaka 2021;

(ii) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 4 wa Mwaka 2021;

(iii) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usajili wa Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu wa Mwaka 2021;

(iv) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji wa Mwaka 2021. Marekebisho haya pia yanakusudia kuhakikisha kwamba shughuli za zimamoto na uokoaji nchini zinafanyika kwa ufanisi ili kuendelea kuwavutia wawekezaji kwa kuwashakikishia usalama wa maisha na mali zao; na

(v) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 5 wa Mwaka 2021.

Mheshimiwa Spika, nirejee tena kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao mizuri iliyotolewa wakati wa kujadili Miswada hiyo muhimu ambayo itasaidia sana kuondoa mapungufu yaliyobainika sambamba na kuboresha baadhi ya masharti katika utekelezaji wa sheria hizo. Serikali itafanya kazi maoni na ushauri uliotolewa kwa lengo la kuhakikisha kwamba utekelezaji wa sheria hizo unawanufaisha Watanzania.

Mheshimiwa Spika, niwapongeze na kuwashukuru Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri kwa kazi nzuri ya kuwasilisha Miswada ilijojadiliwa katika mkutano huu pamoja na kutoa ufanuzi mbalimbali wakati wa kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge. Aidha, nimpongeze Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na wataalamu wake kwa kazi nzuri ya kuandaa Miswada iliyowasilishwa katika mkutano huu.

Mheshimiwa Spika, maeneo ya msisitizo kisekta. Jukumu langu la msingi lillilonisimamisha mbele ya Bunge lako Tukufu ni kutoa maelezo mafupisana hususan kuhusu shughuli za Mkutano huu wa Nne wa Bunge kabla ya kuahirishwa. Hata hivyo, kabla ya kuhitimisha Mkutano huu, naomba niweke msisitizo wa baadhi ya masuala kwa viongozi, watendaji na wananchi kwa ujumla wao katika kutekeleza majukumu yao ya kuwaletea maendeleo.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya maeneo ambayo nitayatolea msisitizo hapa ni suala la tozo na uendelezaji wa miundombinu ya afya ya msingi, maandalizi ya uandikishaji wa wanafunzi wa kidato cha kwanza ifikapo Januari 2022, Mfumo wa Stakabadhi Ghalani, unaotumika kwenye masoko ya mazao, ununuzi wa mazao yenyewe ya nafaka, tahadhari dhidi ya UVIKO-19, lakini pia na matumizi ya mitandao na mwisho michezo.

Mheshimiwa Spika, uendelezaji wa miundombinu ya afya ya msingi. Serikali inatekeleza Sera ya Afya ya mwaka 2007 yenyе lengo la kuwashirikisha wananchi katika ujenzi wa vituo vya afya na zahanati. Azma ya Serikali ni kuona kila Kata inapata kituo cha afya na kila kijiji kinakuwa na zahanati ili kusogeza huduma hizo karibu na wananchi na kuwaondolea adha ya kusafiri umbali mrefu. Hadi sasa, Tarafa 363 zilizopo Tanzania Bara zina vituo vya afya vyenye uwezo wa kutoa huduma za upasuaji za dharura, huduma za mionzi na maabara za kisasa pia zimejengwa.

Mheshimiwa Spika, ili kuzifikia Tarafa nyingi zaidi, Serikali imeamua, kwanza, kuzitambua kata za kimkakati na tarafa zote ambazo hazina vituo vya afya. Pili, kutumia fedha zitokanazo na Tozo za Miamala ya Simu kujenga vituo vya afya vya kimkakati ambavyo vitakuwa na uwezo wa kutoa huduma za upasuaji za dharura, huduma za mionzi na maabara za kisasa katika kata za kimkakati na makao makuu ya tarafa hizo.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa Serikali imeshapeleka shilingi bilioni 37.5 zilizotokana na makusanyo ya Tozo ya

Miamala ya Simu kwenye Halmashauri kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya kwenye Tarafa 150 kati ya 207. Kila Kituo cha Afya kimepelekewa shilingi milioni 250 za awali kwa ajili ya kuanza ujenzi huo. Natoa maelekezo kwa watendaji wote wa Serikali za Mitaa kuhakikisha kwamba fedha hizo zinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa na kuakisi thamani ya fedha kwenye utekelezaji wa miradi hiyo. Tozo ya (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, maandalizi ya uandikishaji wa wanafunzi wa kidato cha kwanza, Januari 2022. Sote tunafahamu kwamba jana tarehe 9 Septemba, 2021 vijana wetu wa darasa la saba walimaliza mtihani wa Taifa wa Elimu ya Msingi ulioanza tarehe 8 Septemba, 2021. Hivyo basi, nitumie fursa hii kuwapongeza na kuwaombea kwa Mwenyezi Mungu awajaalie wote waliofanya mtihani huo waweze kufaulu vizuri na hatimaye kujunga na kidato cha kwanza, lakini pia waweze kujunga na vyuo vya ufundi na kuijendeze na taaluma nyinginezo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tangu kuanza kwa utekelezaji wa Sera ya Elimu Msingi Bila Ada kumekuwa na mwitikio mzuri wa mahudhurio ya wanafunzi na hivyo kuongeza idadi ya wahitimu katika mitihani ya kujipima na kumaliza elimu ya msingi. Ongezeko hilo la idadi ya wahitimu limesababishwa na changamoto ya kutokuwepo kwa miundombinu ya elimu ya kutosha hususan madarasa ya kuweza kuwapokea wahitimu wa darasa la saba wanaofaulu kujunga na kidato cha kwanza.

Mheshimiwa Spika, kufuatia hali hiyo, Serikali ilitoa maelekezo kwa watendaji wa Serikali za Mitaa kuhakikisha wanatumia takwimu zilizopo kupanga maoteo na kutenga fedha katika mipango yao ya bajeti za kila mwaka ili miundombinu ya elimu, samani na shule hitajika ziwepo kwa wakati. Maelekezo haya, yalilenga kuiwezesha Serikali kutambua mahitaji ya miundombinu ya elimu yatakayokidhi idadi hiyo ya wanafunzi na hivyo kuhakikisha miundombinu hiyo inaandaliwa mapema. Katika mwaka huu 2021, makadirio yanaonyesha kuwa wanafunzi 934,706 sawa na asilimia 83.68 ya wanafunzi 1,115,041 waliohitimu mtihani wa

darasa la saba wanatarajiwa kujunga na kidato cha kwanza ifikapo Januari, 2022.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na uhaba wa vyumba vya madarasa katika shule za sekondari, Serikali imetumia shilingi bilioni 33.73 kwa ajili ya kujenga maboma 2,699 kati ya maboma 4,539 ya vyumba vya madarasa kwenye maeneo mbalimbali nchini. Fedha hizo zinatokanana Tozo ya Miamala ya Simu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba kuititia fedha za tozo tayari Serikali imepeleka shilingi bilioni saba kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma 560 ikiwa ni awamu ya kwanza. Aidha, maboma 1,840 yatakayogharimu shilingi bilioni 23 yatakamilishwa kuititia ruzuku ya Serikali Kuu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kurejea maelekezo niliyoyatoa wakati nafunga mafunzo elekezi kwa Wakuu wa Mikoa na Makatibu Tawala wa Mikoa kwamba wahakikishe miundombinu hiyo inakamilika kwa wakati. Lengo la Serikali ni kuona vijana wote waliofaulu kujunga na kidato cha kwanza mwakani wanapokelewa na kuanza masomo yao kwa asilimia mia moja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, bei elekezi ya mafuta. Tarehe 31 Agosti, 2021 Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati Nchini (*EWURA*) ilitangaza bei mpya elekezi kwa bidhaa za mafuta kwa mwezi Septemba ambapo ilionesa kupanda kwa bei za bidhaa hizo. Kufuatia taarifa hiyo na malalamiko ya wananchi juu ya kupanda kwa bei za bidhaa hizo, tarehe 1 Septemba 2021, Serikali ilisitisha bei mpya zilizotangazwa na *EWURA* ili kufanya mapitio ya kina ya kupanda huko kwa bei hizo.

Mheshimiwa Spika, tulichukua hatua kutokana na ukweli kwamba kupanda kwa bei ya mafuta kunawaumiza wananchi hususan wale wa hali ya chini. Kwa kilitambua hilo, tarehe 2 Septemba, 2021, niliunda timu maalumu ya uchunguzi inayoongozwa na Mheshimiwa Tabasam, Mbunge wa Sengerema. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na mambo mengine, timu hiyo inafuatilia kupanda kwa bei za bidhaa za mafuta mara kwa mara hususani petroli, dizeli, mafuta ya taa na ndege na kisha kuishauri Serikali hatua stahiki za kuchukuliwa. Aidha, nimeielekeza timu hiyo ijiridhishe kuhusu utitiri wa tozo kwenye bidhaa za mafuta na kuja na mapendekezo ya namna nzuri ya kulishughulikia suala hilo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa timu hiyo tayari imeanza kutekeleza majukumu yake tangu tarehe 2. Pia itakapokamilisha taarifa yake Serikali itatoa mwelekeo wa yale yatakayopendekezwa.

Mheshimiwa Spika, Mfumo wa Stakabadhi za Mazao Ghalani na Ushirika. Miiongoni mwa maeneo ambayo Serikali inayapa msukumo wa kutosha ni masoko na mifumo ya mauzo ya mazao ya wakulima. Serikali inachukua hatua hizi ili kuhakikisha kuwa wakulima wanapata tija na kunufaika na mazao yao. Katika kutimiza azma hiyo, Serikali imeondoa mifumo isiyo rasmi ya ununuzi wa mazao ambayo imekuwa ikiwakandamiza wakulima na kuwanufaisha baadhi ya wanunuzi wasiokuwa waaminifu. Mathalan, tumeondoa mifumo holela kama vile kangomba, butula, chomachoma, katafunua, kula maua, njemke na mifumo mingineyo ambayo ilikuwa inampunja na kumnyonya mkulima. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kwa mantiki hiyo, Serikali imekuwa ikisimamia kikamilifu mfumo wa stakabadhi za mazao ghalani ambao umeonesha mafanikio makubwa katika uuzaaji wa mazao yakiwemo korosho, ufta, dengu, choroko na kakao. Kwa lugha nyingine, ufanisi wa mfumo huo, umekuwa kichocheo katika kupunguza umaskini na kuongeza uchumi wa nchi na wakulima mmoja mmoja kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, taarifa zinaonesha kuwa kuuza mazao kupitia mfumo wa stakabadhi ghalani na ushirika kunatoa nguvu ya pamoja kwa wakulima katika upatikanaji wa masoko sambamba na kuimarisha bei ya mazao husika. Minada iliyofanyika hivi karibuni imesaidia kuongezeka kwa

bei ya mazao yaliyotumia mfumo wa stakabadhi ghalani ikiwemo korosho, ufuta, dengu, choroko na kakao.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2020 bei ya choroko iliongezeka kutoka Sh.600 kwa kiwango cha chini hadi Sh.800 kiwango cha juu kwa kilo na kufikia shilingi 900 hadi shilingi 1,300 kwa kilo katika Vituo vya Magu, Uzogele, Igunga na Manyoni. Kadhalika, hivi karibuni tumeona bei ya kakao Wilayani Kyela na Wilaya ya Busokelo ikiongezeka maradufu kutoka shilingi 2,500 hadi shilingi 5,000 kwa kilo baada ya kutumia mfumo wa stakabadhi ghalani.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo, natoa maelekezo kwa Wizara ya Kilimo kushirikiana kwa karibu na Vyama vya Ushirika na Vyama vya Msingi katika kuhakikisha wanawawezesha wakulima kupata elimu na manufaa ya kutumila mfumo wa stakabadhi ghalani bila usumbufu ili waweze kuwapatia tija.

Mheshimiwa Spika, ni kweli mfumo wa stakabadhi ghalani unahitaji miundombinu ya maghala. Hata hivyo, changamoto hizo zinaendelea kufanyiwa kazi ili mazao mengi zaidi yaingizwe kwenye mfumo huo mwaka hata hadi mwaka mwaka na kuleta tija kadri wanavyoelimishwa wakulima na kuridhia mfumo huo kutumika katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, rai yangu kwa wakulima na wanunuvi wa mazao ni kwamba, mfumo wa stakabadhi ghalani ndiyo pekee uliothibitika na kuonesha matokeo makubwa yenye manufaa. Hivyo basi, tuendelee kuuimarisha katika mazao ya biashara nchini ili kuleta mafanikio kwa wakulima na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, ununuvi wa nafaka nchini; Serikali imefanikiwa kwa kiwango kikubwa kuhamasisha uzalishaji wa mazao ya chakula hususan nafaka pamoja na mazao ya biashara. Ongezeko hili la uzalishaji linakwenda sambamba na jitihada za Serikali za kuimarisha masoko ya ndani ya mazao pamoja na kutafuta masoko ya nje.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuboresha mifumo ya masoko, Serikali inahamasisha ujenzi wa viwanda vya uchakataji wa mazao yanayozalishwa hapa nchini ili kuimarisha bei ya mazao hayo na hivyo kumpatia tija mkulima.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuanza kwa msimu wa ununuzi wa mahindi hususan katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, tulipokea malalamiko ya wananchi kuhusu umbali wa vituo vya kununulia mahindi na bei kutoridhisha. Kama mnavyofahamu, kwa kiasi kikubwa ununuzi wa mahindi nchini hufanywa na wafanyabiashara binafsi. Hata hivyo, ili kuimarisha bei ya mahindi, Serikali hutoa fedha kwa Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (*NFRA*) na Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (*CPB*) ili ziweze kununua mahindi kwa ajili ya hifadhi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, jana tarehe 9 Septemba, 2021 Bunge lako tukufu lilipokea hoja binafsi kutoka kwa Mheshimiwa Justin Nyamoga, Mbunge wa Kilolo na kuungwa mkono na Waheshimiwa Wabunge. Hoja hiyo, ililenga kuishauri Serikali kuingilia kati soko la mahindi ili kunusuru wakulima wa zao hilo.

Mheshimiwa Spika, awali Serikali ilitoa shilingi bilioni 15 kwa ajili kuwezesha Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (*NFRA*) kununua mahindi maeneo mbalimbali kwa ajili ya uhifadhi wa hifadhi yetu ya Taifa ya chakula. Pia Serikali ilitoa kwa Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko shilingi bilioni 10 kuongeza mtaji wa ununuzi wa mazao kwenye bodi hiyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwa kiasi hicho cha fedha ni kidogo ukilinganisha na uzalishaji wa mahindi uliopo hasa kwa msimu huu wa mazao na hivyo, Serikali imesikia kilio cha wakulima kupitia Waheshimiwa Wabunge na kuchukua hatua mbalimbali kuhakikisha kuwa wakulima wa mahindi wanapata soko la mahindi waliyozalisha. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, tayari Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ameridhia kutoa shilingi bilioni 50... (*Makof*)

MBUNGE FULANI: Hatujasikia, irudiwe hiyo.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, mtulie ili tumsikilize Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu kama ungeirudia ile kwanza ili tuisikie wote na hasa wananchi hapa wanakusikiliza kwa hamu zaidi.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, jana tarehe 9 Septemba, 2021 Bunge lako Tukufu lilipokea hoja binafsi kutoka kwa Mheshimiwa Justin Nyamoga, Mbunge wa Kilolo na kuungwa mkono na Waheshimiwa Wabunge. Hoja hiyo, illenga kuishauri Serikali kuingilia kat i soko la mahindi ili kunusuru wakulima wa zao hilo.

Mheshimiwa Spika, tayari Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mama msikivu, mwelewa, ametoa fedha shilingi bilioni 50 ili ziweze kununua zao hilo na ununuzi utaanza Jumatatu tarehe 13 Septemba, 2021. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naiagiza Wizara ya Kilimo kusimamia kwa karibu *NFRA* na *CPB* ili zinunue mahindi ya wakulima pekee, tena watoke ndani ya nchi. Aidha, ongezeni vituo vya kununulia mahindi hadi wilayani na kwenye miji midogo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pia naiagiza Wizara ya Kilimo iendelee kutafuta masoko ya mahindi kwa kukamilisha mikataba mipy ya ununuzi wa mahindi na nchi za Sudan Kusini, DRC na Zimbabwe.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imeruhusu wafanyabiashara kutafuta masoko ya nje ya nchi ambapo vibali vya usafirishaji hutolewa kuitia Ofisi za Wakuu wa

Wilaya kwa lengo la kuwa na kumbukumbu ya kiwango cha mahindi yanayotoka na kiwango cha fedha za nje zinazoingia nchini. Aidha, uuzaji wa chakula nje ya nchi utafanywa kwa umakini mkubwa ili kuhakikisha nchi inaendelea kuwa na hifadhi ya kutosha ya chakula chake. Niendelee kusisitiza Wizara kushirikiana na Sekta Binafsi katika kuongoza, lakini kuongeza thamani ya mazao yetu ikiwemo mazao ya nafaka badala ya kuyauza nje yakiwa hayajaongezwa thamani.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine, Serikali inafuatilia mwenendo wa upatikanaji wa pembejeo ya mbolea ili kuhakikisha bidhaa hiyo kwanza inapatikana kwa wingi na bei nafuu. Lengo la Serikali ni kuwezesha wakulima kumudu gharama za maandalizi ya msimu ujao wa kilimo hasa kwa upatikanaji wa mbolea.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Mji Mpya wa Serikali; Serikali inaendelea na ujenzi wa Mji wa Serikali, mradi ambao unatekelezwa kwa ufanisi mkubwa. Itakumbukwa kuwa katika awamu ya kwanza, Wizara 23 zilijenga ofisi zake na kuhamishia watumishi wapatao 18,300 hapa Jijini Dodoma. Aidha, ujenzi wa majengo ya kudumu ya Wizara 23 na Taasisi zake utaanza tarehe 30 Septemba, 2021. Ujenzi huo, utahusisha ipasavyo kampuni za ujenzi za umma na binafsi ili kuharakisha majengo hayo kukamilika mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kumshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuridhia shilingi bilioni 300 zitumike katika awamu ya pili ya ujenzi huo. Kadhalika, shilingi bilioni 300 nyingine zitatolewa kadri ujenzi unavyoendelea ili kujiridhisha kuwa majengo hayo yanakamilika kwa wakati. Hivi sasa, ujenzi wa miundombinu wezeshi ikiwemo barabara za lami, maji safi na maji takaa, umeme, usambazaji wa mfumo wa gesi, mifumo ya TEHAMA, huduma za zimamoto na upandaji wa miti unaendelea vizuri na kwa kasi kubwa kwenye maeneo ya Mji Mpya wa Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tahadhari dhidi ya UVIKO-19; Tanzania na dunia kwa ujumla bado imeendelea kupambana na ugonjwa wa virusi nya korona maarufu kama UVIKO-19. Janga hili limesababisha baadhi ya ndugu zetu kupoteza maisha na wengine kuendelea kuugua. Hivyo basi, hatuna budi kuendelea kuchukua tahadhari kwa kujikinga na maambukizi ya UVIKO-19.

Mheshimiwa Spika, nawasihi Waheshimiwa Wabunge wenzangu na wananchi wote, tufuate maelekezo yanayotolewa na watalam wa afya na pale mtu anapoona dalili ambazo hazieleweki, awahi kwenye kituo cha kutolea huduma za afya kilicho karibu ili afanyiwe uchunguzi na kupatiwa matibabu.

Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine ya kukabiliana na UVIKO-19, tarehe 28 Julai, 2021, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alizindua rasmi kampeni ya chanjo dhidi ya ugonjwa huo. Hivi sasa, chanjo hiyo inapatikana maeneo yote nchini katika vituo mbalimbali nya kutolea huduma ya afya wilayani na mikoani.

Mheshimiwa Spika, niwatoe hofu Waheshimiwa Wabunge wenzangu na watanzania wote kuwa chanjo hii ni salama na haina madhara yoyote. Chanjo hiyo ambayo imethibitishwa na watalaam na maabara zetu, ni hiyari lakini ni muhimu sana kuchanja kwa sababu inasaidia kuongeza kinga ndani ya mwili. Hivyo, niwaombe twendeni tukachanje ili kukabiliana na janga hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, matumizi ya mitandao; hivi karibuni kumejitokeza tabia ya baadhi ya watu kutumia vibaya haki ya uhuru wa mawazo na mifumo mbalimbali ya mawasiliano. Matumizi mabaya ya mitandao yamesababisha kusambazwa kwa taarifa za upotoshaji, kashfa za kutisha, zaidi kuwatishia watu na wakati mwingine kudhalilisha watu, vikundi au viongozi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika kulinda na kutunza usalama, amani, maadili, umoja na mshikamano wa nchi, nawaagiza Mawaziri wa Mambo ya Ndani, Waziri wa Katiba na Sheria, Waziri wa Utumishi, Waziri wa Mambo Nje, Waziri wa Habari na Teknolojia ya Mawasiliano kutumia sheria, kanuni na taratibu zilizopo kuhakikisha kwamba vitendo na matumizi mabaya ya mtandao vinathibitiwa hapa nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Michezo; nyote mtakubaliana na mimi kwamba kumekuwepo na mwamko mkubwa sana wa masuala ya sanaa, burudani na michezo hapa nchini. Hivi sasa, michezo imekuwa chanzo kikubwa cha biashara, utalii, kuimarisha afya na ajira kwa vijana wetu. Kwa kuzingatia hilo, Serikali imeendelea kuchukua hatua za makusudi za kukuza michezo nchini. Hatua hizo zinahusisha kuundwa kwa Mfuko wa Maendeleo ya Michezo na kurejesha mashindano ya UMITASHUMTA, UMISSETA na SHIMIWI. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuridhia kuanzishwa kwa Mfuko wa Maendeleo ya Michezo nchini na kukubali kudhamini mashindano ya wanawake *CECAFA* yajulikanayo kama *Samia Cup* ili kutoa motisha kwa wanawake kushiriki zaidi katika michezo. Mashindano hayo, yanayojulikana kama *Samia Cup* kwa wanawake yanaendelea sasa hivi nchini Kenya, sambamba na mashindano ya *Kagame Cup* kwa upande wa wanaume yaliyohitishwa wiki mbili zilizopita. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuanzishwa kwa Mfuko ni jambo jema, Mfuko huo utasaidia upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kuziandaa vyema timu zetu za Taifa za michezo mbalimbali na kuziwezesha kushiriki katika tija mbalimbali ya mashindano na michezo ya kimataifa. Pia utatumika kuimarisha miundombinu ya michezo na upatikanaji wa vifaa vya michezo, kuendeleza na kuwezesha shule na vituo vya umahiri wa michezo, kuendesha programu za mafunzo ili

kupata wataalam wa kutosha, kuwezesha programu za michezo kwa jamii na mashindano ya kitaifa na kimataifa.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyotangulia kueleza, michezo ni biashara na imekuwa chanzo muhimu cha ajira hususani kwa vijana. Aidha, ibara ya 243 ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020, inaielekeza Serikali kuanzisha mfumo thabiti wa michezo ya kulipwa ili kulinda na kuendeleza vipaji vilivyopo kwa manufaa ya Taifa letu na vijana wetu kujipatia ajira kwa kutumia vipaji vyao. Tayari, Sheria ya Baraza la Michezo la Taifa imefanyiwa mabadiliko na kuruhusu michezo ya kulipwa na baadhi ya timu zetu zimeshaanza kutumia sheria hiyo na mfumo huo.

Mheshimiwa Spika, kutohana na utekelezaji wa sheria hiyo, hivi karibuni, tumeshuhudia watalaam wa michezo na wachezaji kutoka mataifa makubwa yaliyoendelea kimichezo wakija hapa nchini kwetu kutafuta fursa ya ajira kupitia michezo. Lakini vilevile, tumeshuhudia uwekezaji mkubwa kwenye vilabu vyetu vikubwa nchini hususani Azam, Simba na Yanga na kuvifanya vilabu hivyo kuendeshwa kibiashara zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kwanza kuupongeza Uongozi wa Shirikisho la Soka Tanzania (*TFF*) chini ya Rais Wallace Karia kwa usimamizi mzuri wa soka nchini.

Pia niwapongeze sana wawekezaji na watendaji wa Vilabu vya Azam, Simba na Yanga kwa uwekezaji mkubwa na usimamizi mzuri wa vilabu hivyo kwenye soka letu ambao umeanza kuzaa matunda.

Mheshimiwa Spika, nataka niwahakikishie wadau na wapenzi wa michezo kuwa, Serikali itaendelea kuimarisha na kuvutia uwekezaji mkubwa katika tasnia ya michezo. Lengo ni kuibua na kuendeleza vipaji vya vijana wetu kimichezo ili wawewe kushindana katika masoko ya michezo ya ndani na nje ya nchi na hivyo kuimarisha ajira, mapato yatokanayo na shughuli za michezo pamoja na mchango wa sekta ya michezo katika pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuipongeza timu yetu ya Taifa ya Mpira wa Miguu (*Taifa Stars*) kufuatia ushindi wa mabao matatu kwa mawili dhidi ya Madagascar jana na hivyo kuongoza Kundi J, katika hatua ya pili ya kufuzu kucheza Kombe la Dunia mwakani nchini Qatar. Pia, timu yetu ya Taifa ya wanawake Twiga *Stars* itakayoshiriki mashindano ya *COSAFA* nchini Afrika Kusini kuanzia tarehe 28 Septemba, 2021. Vile vile navitakia kila la heri Vilabu vyetu vya Azam, Biashara *United*, Simba na Yanga katika uwakilishi wao kwenye michuano ya Shirikisho na Ligi ya Mabingwa ya Chama cha Soka Barani Afrika - *CAF*.

Mheshimiwa Spika, vilevile tunaitakia kila la heri timu yetu ya wanawake ya Kriketi inayoshiriki mashindano ya kufuzu kushiriki Kombe la Dunia la Michezo huko Nchini Botswana, pamoja na kuitakia mafanikio mema timu yetu ya mchezo wa wavu inayoendelea kushiriki mashindano ya Afrika ya mchezo huo Nchini Rwanda, huku tukisubiri mashindano ya *CRDB Basketball Cup*, yatakayoanza mwezi Oktoba hapa Jijini Dodoma ikishirikisha timu za mikoa yote ambazo kwa sasa wanaendelea na maandalizi.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kukipongeza sana Kituo cha Azam (*Azam Media*) hususan upande wa matangazo ya runinga kwa kuuibua na kuutangaza vyema mchezo wa masumbwi nchini. Juhudi hizi za *Azam Media* wakishirikiana na wadau wengine zimevezesha kuwaibua wanamasumbwi wetu hapa nchini na kutumia vizuri fursa hiyo kukuza vipaji vyao. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana mabondia wetu Twaha Kiduku kwa kumtwanga Dulla Mbabe katika pambano lilitovuta hisia za Watanzania wengi. Vilevile, nimpongeze sana bondia Hassan Mwakinyo kwa kumdunda mpinzani wake Mnamibia Julius Indongo kwa *knock out* na kutetea mkanda wake wa Chama cha Ngumi Afrika (*ABU*). Wanamasumbwi wetu wameendelea kuifanya Tanzania itambulike zaidi ulimwenguni. Sasa Watanzania tunasubiri pambano la watani kati ya Mwakinyo na Kiduku, hatujui ni lini litatokea. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nihitimishe hotuba yangu kwa kumshukuru Katibu wa Bunge na Watendaji wa Ofisi ya Bunge kwa kazi kubwa ya kuratibu vikao vya Mkutano huu. Aidha, niwashukuru Watendaji wa Serikali kwa kufanikisha shughuli zilizopangwa na Bunge lako Tukufu kwa weledi na ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, kipekee, niwashukuru wanahabari kwa kufikisha habari kuhusu mkutano huu kwa wananchi. Navishukuru pia vyombo vya ulinzi na usalama kwa huduma wanazozitoa kwa washiriki wa Bunge hili bila kuwasahau madereva waliohudumia wakati wote tukiwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, natambua kuwa baada ya Mkutano huu Waheshimiwa Wabunge wenzangu watakuwa wakirejea majumbani kwao kwa ajili ya kuendelea na shughuli za kuwahudumia wananchi ikiwa ni pamoa na kuwaeleza mambo yaliyojiri hapa Bungeni. Kwa hiyo, niwatakie safari njema na niwaombe kuwa wakawaeleze wananchi pia kuhusu matarajio yetu kwao na kuwasihii waendelee kumuunga mkono Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, pia kuiunga mkono Serikali yetu katika kusukuma mbele gurudumu la maendeleo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tarehe 19 Oktoba, 2021, ikitegemewa na mwandamo wa mwezi Mtukufu, ndugu zetu Waislamu wataadhimisha Mazazi ya Mtume Muhammad (*Swalla Allahu Alayh Wasallam*). Hivyo, nitumie nafasi hii kuwatakia kila la heri katika maandalizi na hatimaye maadhimisho ya shughuli hiyo ya Maulid ya kuadhimisha Mazazi ya Mtume Muhammad (*Swalla Allahu Alayh Wasallam*). (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liahirishwe hadi tarehe 2 Novemba, 2021, siku ya Jumanne, saa tatu kamili asubuhi litakapokutana tena katika ukumbi huu hapa Jijini Dodoma.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofî*)

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

SPIKA: Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri sana ambayo imetolewa. (*Makofî*)

Tunakushukuru sana kwa kweli kwa hotuba yako ambayo *ime-summarize* mambo ambayo tumeyafanya hapa Bungeni ikiwemo taarifa njema kadhaa na kipekee ikionesha kazi nzuri ambayo Waheshimiwa Wabunge mmefanya, hasa kuhusiana na hoja ya soko la mahindi ambalo kwa niaba yenu nipeleke salamu za shukrani nyingi sana kwa Rais wetu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, ambaye kupitia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu hapa tumejulishwa kwamba zimetengwa shilingi bilioni 50 kwa ajili ya ununuzi wa mahindi. Naamini habari hii ni njema mno kwa watu wetu. Ni njema sana, huwezi kupata picha. Wakulima kule Songea, Katavi, Rukwa na maeneo mengine nchini, habari hii ni habari inayotia moyo sana sana.

Mheshimiwa Waziri Mkuu tupelekee salamu kwa Mheshimiwa Rais, tunamshukuru sana. (*Makofî*)

Waheshimiwa Wabunge, uongozi wa Mkoa wa Dodoma, kipekee Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa anawatangazia Wabunge ambao watakuwepo tarehe 14, keshokutwa hapa Dodoma kwamba kutakuwa na shughuli maalum ya Mpango Mkakati wa Uelimishaji na Uhamasishaji wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 ambao utazinduliwa na Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan katika Viwanja vya Jamhuri hapa Dodoma. Kwa hiyo, watakaokuwepo tarehe 14, basi tuungane na Mheshimiwa Rais hapa kwenye viwanja vya Jamhuri Dodoma kuanzia saa 2.00 asubuhi.

Pia Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunashukuru sana kwa ujenzi wa Ofisi za Makao Makuu ya Wizara mbalimbali ambao utaanza keshokutwa hapa Dodoma, tarehe 30 Septemba, 2021. Pia ni shukrani kubwa kwa Mheshimiwa Rais kwa kutenga shilingi bilioni 300 kwa ajili ya zoezi hilo. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais. (*Makof*)

Waheshimiwa Mawaziri tumuunge mkono Mheshimiwa Rais. Habari ya semina, kongamano Dar es Salaam na nini, imepitwa na wakati. Dodoma ni Makao Makuu ya Nchi kisheria. Siyo kwa hiari, siyo kwa nini; na msidhani kwamba vitu hivi vinapendeza. Yaani wananchi wa Tanzania ni watu walioelimika sana, wana uwezo mkubwa sana wa kufikiri na kuona. Kwa hiyo, mnayoyafanya haya hayawajengei heshima sana. Hatusemi kwamba Dar es Salaam kusifanyike chochote, lakini kuna wakati najiuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu, hivi nani ana-control *Government expenditure?* Maana yake semina Dar es Salaam magari yanakwenda huko, halafu baada ya siku mbili yanarudi tena Dodoma; hayakai siku mbili Wizara nyiningine hao wanakwenda Dar es Salaam na kurudi tena Dodoma. Vikao hivi vifanyikia Dodoma, una-cut *expenditure* kwa kiwango kikubwa sana kwa sababu wahusika wengi hawatalipwa chochote. Ila hao hao wakienda Dar es Salaam; madereva, wao wenyewe, wasaidizi wao na nani, wote ni posho, posho, posho. Halafu mwisho wa siku likitajwa neno “posho”, ni Wabunge tu. (*Kicheko/Makof*)

Kwa hiyo, tu-cut costs kwa kiwango kikubwa. Nchi yetu inahitaji fedha nydingi, mkiangalia matatizo huko vijijini; Januari tunatakiwa sijui madarasa mangapi ya *form one* nchi nzima Mheshimiwa Ummy anajua. Ni shughuli pevu kujenga madarasa hayo, madawati yake, kuajiri walimu na vifaa vingine na kadhalika. Maeneo yetu mengi sana yanahitaji fedha nydingi, kwa hiyo, ni vizuri sana kujaribu kubana.

Wizara ya Fedha fanyeni *tracking expenditure* muone, halafu mwisho wa mwaka tujaribu kuangalia ni Wizara gani inayoongoza katika *unnecessary expenditures* ambazo zingeweza kuwa *saved* kwa uamuzi tu fulani wa busara. Kwa

sababu ni fedha nyingi sana, *it's a lot of money* kwa mwaka ukiaangalia.

Mwisho, nami niungane na Mheshimiwa Waziri Mkuu kuwatachia kila la heri timu zetu zenyé mechí za Kimataifa; KMKM, Biashara; nani wengine? Azam, halafu *of course* Simba ndio wenyewe na wale wengine pia. Tunawatachia kila la heri. Wengine keshokutwa Jumapili mtihani unaanza, basi tutakuwa kwenye *TV*tutaangalia wanavyoendelea. (*Makofi/Kicheko*)

Cha muhimu Waheshimiwa Wabunge, nawaomba mtakaokuwepo Dar es Salaam tarehe 19 ya mwezi huu, basi tuungane pale Kwa Mkapa ili tuweze kuiona shughuli pevu ya *Simba Day*. Maana hiyo shughuli itakuwa ni ile ambayo mtoto hatumwi dukani. (*Makofi*)

Kwa hiyo, tunawaomba sana Waheshimiwa mtakaokuwa Dar es Salaam wakati huo muungane mkono na Spika wenu maana nitakuwepo. Maana ile shughuli alikuwepo Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, walituonea sana. Sasa tunakuja kivingine tarehe 19. (*Makofi*)

Kwa kweli michezo inachangamsha nchi, inatufanya Watanzania tunakuwa wamoja, tunafurahi, amani yetu inazidi kuwa kubwa zaidi. Kupitia michezo tunaweza tukafanya mambo mengi tu makubwa ya kuiweka nchi yetu katika ramani kubwa zaidi hata kiatalii katika nchi yetu. (*Makofi*)

Katibu.

NDG. NENELWA MWIHAMBI, ndc – KATIBU WA BUNGE:
Wimbo wa Taifa na Wimbo wa Jumuia ya Afrika Mashariki.

SPIKA: Ooh, kabla ya Wimbo wa Taifa sijahoji bwana ile Hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, nisije nikasahau. Hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu mmeisikia, kwamba Bunge hili sasa liahirishwe hadi tarehe 2 Novemba, 2021, Jumanne, saa

3.00 asubuhi. Hadi Novemba yaani kuanzia leo, duh, mbali kidogo.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

SPIKA: Dah! Kwa sauti hizi ngoja nitafakari kidogo. Nadhani walioafiki Hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu wameshinda. (*Vicheko/Makofi*)

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

SPIKA: Kwa hiyo, Katibu ameshasema shughuli inayofuata, sasa naomba Kwaya ya Bunge na Waheshimiwa Wabunge nawaomba tusimame.

WIMBO WA TAIFA NA WIMBO WA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI

(Hapa Kwaya ya Bunge iliimba Wimbo wa Taifa na Wimbo wa Jumuia ya Afrika Mashariki)

SPIKA: Makofi kwa Kwaya yetu ya Bunge Waheshimiwa Wabunge. (*Makofi/Vigelegele*)

Ahsante sana, mnatubeba, mnaimbaji vizuri sana, mwendeleze sana juhudhi hiyo. Tunataka ile Kwaya ya Utumishi tuishinde na Kwaya ya Mheshimiwa Jaji Mkuu ile ya Mahakama nayo tuweze kuishinda. Kwa hiyo, nawatakia kila la heri. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, Mwenyezi Mungu awatangulie, mwende salama, mrudi salama. *Inshallah* tutakutana tarehe 2 Novemba, 2021. Ahsanteni sana.

*(Saa 10.30 Jioni Bunge Lilahirishwa hadi Siku ya Jumanne,
Tarehe 2 Novemba, 2021 Saa Tatu Asubuhi)*